


ALIAPA KWA NAFSI YAKE

 Ninahisi kama kwa namna fulani ninaingilia mambo wakati ninaposhuka hapa. Ndugu Neville a—ana ukarimu mwingi sana. Anasema, “Sasa, Ndugu Branham, karibu jukwaani, pamoja na Neno,” na kitu kama hicho. Na, mwajua, kidogo najisikia kama ninapaswa kumsikiliza kwa muda kidogo. Kwa hiyo, nitakaporudi usiku wa leo, mbona, nita—nitamsikiliza. Nita—nitatoa onyo hilo awali. Amina. Naam.

² Ninatumaini kila mtu anajisikia vizuri. Nanyi mwaonekana wazima, na kwa hivyo ninashukuru kwa hilo.

³ Sasa, ni siku mbaya, huko nje, lakini ni kuzuri na kuna joto humu maskanini. Nasi tunashukuru kwa ajili ya paa hili dogo, la kale, na kuta zake nne hapa, ambamo tunakusanyikia, na mahali pazuri, penye joto pa kumwabudia Bwana. Panaweza pasiwe mahali pa—patoshelevu, labda, mahali pa kuabudia, kama walivyo napo huko kwingine. Lakini Uwepo wa Roho Mtakatifu sikuzote ndio tunaenda, ni kupata Uwepo Wake, ndio unaolileta nafsini mwe—mwetu.

⁴ Sasa, kama ndugu alivyosema, “Hii ni siku mbaya, na kunateleza sana barabarani.” Mimi pamoja na Billy, huko nyuma, hivi punde tumeendesha gari maili mia tisa za barabara inayoteleza. Huku—huku tukienda tu mwendo wa maili kumi na mbili, kumi na tano, si zaidi ya maili thelathini kwa saa, wakati wowote, tukisonga mbele tu; mabasi yamekwama kwenye mitaro, na kadhalika. Kwa hiyo tunajua ni vigumu sana, kuendesha gari, nyakati hizi.

⁵ Kwa hiyo sasa, kikundi kidogo chenu, kama mnataka kusonga mbele, mbona, popote mnapoweza kusikia vizuri, vema, hiyo ni—hiyo ni sawa kabisa.

⁶ Sasa, jana jioni, ni—ningeninii...nilikuwa na shughuli nyingi sana. Nami ningalimpigia simu Ndugu Neville, kumwambia, ama kwa ajili ya kipindi chake, na kadhalika. Tungeingia, asubuhi ya leo, na kuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa, na kadhalika. Lakini sikuweza kumfikia, kwa sababu nimekuwa na shughuli nyingi, nyingi sana tangu niliporudi. Pia ninajiandaa kuondoka tena sasa, kwenda Chicago, kwa ajili ya mikutano kule. Na tutaendelea hadi Phoenix na Pwani ya Magharibi.

⁷ Sasa, tulikuwa na mkutano mzuri sana huko Bing... Binghamton. Binghamton, New York. Siwezi kulitamka hilo. B-i-n-g-h-a-m-t-o-n. Ni Bing...[Mtu mmoja anasema, “Binghamton.”—Mh.] Binghamton. Uh-huh. Na ni ninii... Ninataka kulitamka Bing-ham-ton. B-i-n-g h-a-m t-o-n, mnaona, Bing-ham-ton. Lakini wanauita tu Binghamton. Uko

sawa, Ndugu Johnny. [Ndugu mmoja anasema, “Jamaa zangu wanaishi moja kwa moja karibu na hapo.”] Loo, kweli? Vema, hilo ni jema. Tulikuwa kwenye Ukumbi wa Endicott. Naam, mnajua mahali huo ulipo, katika Mji wa Johnson.

⁸ Tukawa na...bila shaka mkutano wa ajabu sana huko juu; kurukia tu moja kwa moja, upesi, mwajua, na—na bila maandalizi. Walipiga simu tu siku moja. Na sehemu hizo zote za kutembelea, hata hivyo Roho Mtakatifu akasema, “Panda huko juu.” Nami nikaona kile ilichokuwa. Ilikuwa ni miongoni mwa kundi, Wakatoliki wengi sana mle ndani, na kadhalika, na bila shaka ilikuwa ni kifungua macho kikubwa kwa watu hao.

⁹ Na sasa walininii tu...na kule juu yapata siku sita ama saba usiku, mpaka wana njaa na kiu kabisa. Na—nao wanataka kuandaa mkutano, ama kupiga hema, na turudi kwa ajili ya huo. Mnajua jinsi ilivyo. Kwa hiyo nikawaambia, ama nitapanda nije, ama niwatume baadhi ya ndugu zangu, Ndugu Beeler ama baadhi ya hao wengine waliotaka kupanda kule kwa mkutano wakati mmoja pamoja nao, kule juu.

¹⁰ Sasa, naongozwa sana, bila shaka. Daima, moyo wangu bado unawaka kwa ajili ya nchi za ng’ambo. Laiti tu, kwa namna fulani, baada ya hii ibada asubuhi ya leo, ningekuwa niondoke kwenda Afrika ama India, mahali fulani. Kuona hilo, hitaji kubwa la watu katika nchi hiyo; na jinsi walivyo na upendo mwingi, nao wanataka kuipokea Injili, sana sana, mwajua. Huko, hawana tofauti tulizo nazo huku, mwajua, kuninii...mwajua, kubishania mambo madogo mbalimbali. Wa—wa—wanataka tu kusikia habari za Bwana Yesu. Na hao ndio aina ya watu ambao ungetaka, ungetaka ku—kuwapelekea Ujumbe. Na urahisi huo wake, namna hiyo, vema, huwafanya tu kuwa...Wanalipenda tu. Na haidhuru unasema nini, kama ni jambo fulani kumhusu Bwana, wanataka kujua kulihusu, upesi sana. Na, bila shaka, hapa Marekani, sote tunatofautiana, na ndiyo tunayoita, “mabishano ya bure.” Hiyo ni kweli? Kitu kama hicho. Naam.

¹¹ Jambo lingine, nilipokea simu kadhaa kutoka kwa wachungaji, wakiniambia tu kuhusu ndugu mmoja aliyeandika kitabu. Na hiyo kidogo ilinhangaiisha sana. Sasa, hiyo ni sawa. Simjui huyo ndugu, wala yeye hanijui. Basi hiyo ni sawa. Labda huyo ni ndugu mzuri, na ni kutokuelewa tu, mwajua. Mnajua jinsi mtu...Unaweza kufikia hilo kwa urahisi, wajua, kutoeleweka tu kwa namna fulani. Lakini, tunaamini katika uponyaji wa Kiungu na kuwaombea wagonjwa. Na, labda, huyo ndugu anaamini, pia, lakini ananinii tu...Mnajua jinsi ilivyo, wanapata tu kutolewa kidogo namna hiyo. Na sijawahi kukutana na huyo ndugu mpendwa. Kama ningezungumza naye, naye azungumze nami, labda tungependana, mnaona. Kwa hiyo, haiteti tofauti yoyote, hata hivyo.

¹² Sasa, kwa hiyo sasa, katika Injili, tunataka kufungua, kusoma kidogo, asubuhi ya leo, kutoka katika *lile* Neno. Je, hamlipendi *lile* Neno? Naam. Hilo, hilo Ndilo.

¹³ Sasa, katika . . . Tumekuwa katika mlango wa 10, kwa miezi minne ama mitano iliyopita, naamini. Na kwa hivyo nilianza, asubuhi ya leo, niliwazia, “Vema, sasa, vipi kama Ndugu Neville angeniita niseme jambo fulani asubuhi ya leo? Ningeachia wapi, katika mlango wa 10?” Ndipo nikaanza kuangalia, nami nikamaliza mlango wa 10, baada ya miezi kadhaa.

¹⁴ Kwa hiyo nikasema, “Naam, nitaanza na mlango wa 11.” Ndipo ilitokea niliangalia mle, na huo ndio mojawapo wa ninayoipenda sana, mwajua, nilihofu nitaninii. . . Nikasema, “La, sitaanzia hapo, maana nitakaa humo miaka miwili, kwa kila mmoja.” Kila mmoja wa hao hapo, mabingwa wa imani, mwajua. Jinsi sisi. . .

¹⁵ Kuchukua mlango huo wa 11, kuihalalisha, ingetubidi kurudi nyuma na kupata mwanzo wa uumbaji, na kuushusha huo chini; hiyo ingechukua machache, majuma matatu. Na halafu, Henoko, jinsi alivyotembea na Bwana; hiyo ingechukua majuma mengi kiasi, mwajua, kuondoka kwenye hivyo vifungu viwili. Na halafu huyu hapa Nuhu anakuja, baada ya hapo. Na kisha Ibrahimu, na kuendelea. Loo, jamani! Tungaliwahi kumfikia Ibrahimu, ni—ni vigumu kusema tungekuwa humo ndani kwa muda gani. Tungekuwa tukilichambua huku na huku, na huku na huku. Na, kwa hiyo, juu ya somo kama hilo, inapaswa kuwa ni wakati ambapo tuna uamsho, na mfululizo wa masomo kama hayo, kuendelea tu na mlango wa 11.

¹⁶ Kwa hiyo nikawazia, “Vema, tulienda kule, nami nikaanza na mlango wa kwanza, huo unasikika mzuri sana.” Ninapenda mafundisho ya Waebraia kwa sababu ni—ni ya kina na ni matamu sana. Na mimi—mimi nina hakika ninyi nyote mnayapenda hayo.

¹⁷ Kwa hiyo, niliwazia tungenesoma kidogo tu kutoka kwenye mlango wa 7, labda, asubuhi ya leo, mkipenda, na kuufungua.

¹⁸ Nasi tutapata msingi kidogo wa mazungumzo yetu. Basi—basi tutaanza sehemu ya hivyo vifungu vichache kwenye huo wa 6 hapo. Kwa namna fulani inaingiana nayo, kwa sababu inahusu somo kuu, la Melkisedeki, Mfalme wa Salemu, kwamba Yeye alikuwa ni nani, na alikuwa na uhusiano gani na Kristo. “Na—na Yeye hakuwa na baba, wala mama; hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake. Kamwe hakuwa na mwanzo. Kamwe hukuanza, wala hataisha. Hakuwa na baba wala mama, hana ukoo. Na Yeye—Yeye alikuwa ndiye Mfalme wa Salemu.” Sijui huyu alikuwa ni Nani, ambaye Ibrahimu alikutana naye, Yule aliyekutana naye. Sasa tutarudi nyuma kidogo.

¹⁹ Lakini, sasa, tunafungua kurasa namna *hii*, mnaona; bali kuna Mmoja tu anayeweza kukifungua, na huyo ni Bwana

Yesu. Sivyoy? “Hakuna yeyote Mbinguni wala duniani, chini ya ardhi, aliyeweza ama aliyestahili kukifungua kile Kitabu, au kuifungua Muhuri wake.” Lakini Yesu alipokuja, alikitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono wa kuume, wa mkono wa Mungu, na kukitwaa kile Kitabu na kuifungua ile Mihuri, kisha akaketi mkono wa kuume wa Mungu. Na—na kuna Mmoja tu awezaye kufanya hivyo. Kwa hiyo sasa kama . . . Yeye pekee Ndiye awezaye kufanya hivyo.

²⁰ Sasa, mawazo yangu yangeenda kombo, loo, labda maili milioni moja. Na mawazo ya mtu mwingine yangeenda mbali sana. Lakini tutatumaini ya kwamba atachukua tu, ajalie—ajalie mawazo Yake yawe yetu, asubuhi ya leo. Hiyo ni kweli? Ndipo basi tutafanya vizuri tuwezavyo, nitafanya, kuyaelezea vizuri sana nijuavyo.

²¹ Sasa, halisomwi awali. Kweli kabisa. Tunakuja tu hapa na kulifungua Neno.

²² Na, ilikuwa kwamba, tulipokuwa tukija na kuwa na masomo haya, tunge—tungeyatafakari awali, kwa ajili ya juma linalofuata, kuuendeleza huo mfululizo. Nami ningeandika Maandiko, ya kila mahali kote katika Maandiko, kila jambo dogo ambalo ningeweza. Juma zima, ningeingia chumbani na kuketi mle, na—na kusoma, na kutafakari, na—na juu ya Neno. Na wakati Roho Mtakatifu akinipa jambo fulani, ni—ningeliandika. Nami ningeketi na kuwazia tena, kisha niliandike, lolote ambalo angeniambia.

²³ Ndipo, Jumapili, ningekuja hapa na kuwa na karatasi zimewekwa pote . . . Nawe ingekupasa kuwa na kibao huko nje, ili kuendana nayo, na kuandika, na unapopata Maandiko. Ndipo, juma zima, watu wangesoma hayo, na kuyajumuisha pamoja. Na kuna vile . . . kuna ninii . . .

²⁴ Somo, mnajua, ni jambo zuri sana, lakini muktadha ndio hulikuza somo, mnaona. Ninii . . . Ni muktadha wa hilo somo. Kwa hiyo, katika hili, sisi—sisi . . . Siku hizi, tunaingia tu na, popote, tu—tunaliachilia tu kwa muda kidogo, na kumtumainia Bwana kutusaidia.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

²⁵ Sasa, Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunashukuru kwa yote ambayo Wewe umefanya. Hasa sana, Bwana, kwa kusamehe dhambi zetu, kuweka magonjwa na mateso mbali na milango yetu, tuna furaha sana kwa hilo. Na majaliwa tuliyo nayo, kukusanyika hapa katika nyumba hii ya Mungu, asubuhi hii ya majira ya baridi kali, kukuabudu katika uzuri wa utakatifu Wako. Loo, jinsi tunavyokupenda, tukijua ya kwamba umetuosha kwa Damu Yako Mwenyewe; na ukatuleta mbele za Mungu, bila dosari, bila lawama, kama viumbe vipya katika Kristo Yesu. Tukitazamia wakati, unaokuja, ambapo tutamwona

jinsi alivyo, na kuwa na mwili kama Wake. Loo, tunaitazamia saa hiyo!

²⁶ Na sasa, kama tulivyokusanyika leo, tunakushukuru kwa kuwa umetupa safari salama kwenda New York, na kurudi. Asante kwa kuwa pamoja na kanisa wakati tukiwa hapa. Na mengi ya mambo, loo, maelfu ya baraka hizo kuu ambazo inatupasa kukushukuru kwa ajili yake! Na Wewe unazijua zote, nasi tunasujudu kukupa sifa.

²⁷ Lichukue Neno, asubuhi ya leo, Baba, libariki sasa. Libariki kanisa. Mbariki mchungaji. Mungu, uwe pamoja naye, na, Ee Mungu, umfanye tu baraka kwa maelfu. Mashemasi wa kanisa, wadhamini, washiriki, walei, wote, kuwa tu pamoja nao, Baba. Walimu wa shule ya Jumapili huko nje pamoja na hao watoto wadogo, kuwa pamoja nao. Na jalia mioyo yao midogo iwake tu, asubuhi ya leo, kwa upendo wa Mungu. Tusaidie, vivyo hivyo, kanisani. Na tuondokapo, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo aliponena nasi njiani?” Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Sasa, katika Waraka wa Waebrania.

²⁸ Na, hapa, ninaona kwa shida sana, chini ya mwanga huu, na kwa sababu mimi si mvulana, tena, mwajua. Ninaanza kuwa mzee.

²⁹ Na hapa siku moja, nilikuwa nikienda kutengenezewa miwani ya rangi, kwa ajili ya uakisi wa theluji. Nilikuwa nikienda safari Afrika, na...La, sa—samahani. Nilikuwa nikipanda kwenda Maine, ama huko Canada, kuwinda. Na uakisi wa theluji, huna budi kuvaa miwani, maana jua linatokeza na kukupofusha tu. Kama vile tu macho yako yanavyouma sana, nawe huna budi kuinamisha kichwa chako; ukijaribu kutembea, ukiangalia chini namna *hii*, nayo yanauma. Kwa hivyo, kila wakati ninapovaa jozi, aina yoyote ya miwani ya jua, hunifanya mgonjwa sana hata ni vigumu kwangu kuinua kichwa changu. Na sikuzote ilikuwa hivyo.

³⁰ Kwa hiyo, nikampigia simu Dk. Adair, na nikasema, “Nitumie rangi ya aina gani?” Nikasema, “Nimejaribu kijani, bluu, na nyeusi.”

³¹ Akasema, “Billy, si miwani. Ni macho yako.” Kasema, “Umepita arobaini.”

Nikasema, “Naam.”

Kasema, “Vema, jamani, ni maskini hayo macho yanaharibika.”

Nikasema, “La. Nina macho mazuri.” Nikasema, “Mimi—mimi. . .”

Akasema, “Loo!”

Nikasema, “Loo, naam, naweza.”

³² Kwa hiyo akanituma ng'ambo ya mto, nikachunguzwe macho yangu, mtaalamu fulani. Nikaona hayo yalikuwa ni mapenzi ya Bwana, maana huyo mtu alikuwa Mkristo mashuhuri, na—naye anataka kwenda Afrika pamoja nami nitakapoenda tena. Na mmoja wa madaktari bora sana wa macho huko Louisville, katika Jengo kuu la Heyburn huko. Kwa hiyo alipoyachunguza macho yangu, nayo macho yangu . . .

³³ Aliniingiza kwenye chumba kidogo, na kufungulia kitu fulani, ambapo kulikuwa na giza, na kuniacha niketi pale kidogo, mpaka macho yangu yakapanuka kwake. Na hivyo basi akafungulia kitu kidogo, kasema, "ishirini-ishirini." Vema, ningeweza kusoma kwa kila jicho. Akakifungulia tena, kasema, "kumi na tano-kumi na tano." Nikasoma kutoka kwa kila jicho. Akakiwasha tena, akasema, "kumi-kumi." Niliweza kusoma kwa kila jicho. Kwa hiyo hiyo ilikuwa . . . na huo ndio umbali ungalipaswa kwenda. Kwa hiyo ningeweza kuisoma popote. Hivyo basi—basi akasema . . .

³⁴ Kisha akaiweka juu ya kitu kidogo *hivi*, kisha akachukua kadi ndogo na kuanza kuniletea *hivi*. Ilipofikia papa hapa *hivi*, nikasema, "Samahani."

Akasema, "Vema, umepita arobaini."

Nikasema, "Naam."

³⁵ Kasema, "Kumbe." Kasema, "Una macho mazuri. Lakini mtu, au mwanadamu yeyote aliyepita miaka arobaini, kwa kweli mboni za macho yako huwa bapa. Kama vile, nywele zako huingia mvi. Ni jambo la kimaumbile tu." Kisha kasema, "Yanapokuwa bapa, hayatatanuka kama ipasavyo, namna hiyo." Kisha kasema, "Kitu chochote kilicho karibu na wewe, mboni zako za macho, zinapokuwa bapa, hazitatanuka na kukuruhusu kuona, unaona." Akasema, "Siku moja, unapokaribia," kasema, "itakubidi ukipatie miwani, na kuyaongoza, kuyasoma yote."

Nikasema, "Loo, jamani, daktari!"

³⁶ Na ninaiondoa, mbali *hivi*, kutoka kwangu, ni kamilifu. Lakini ninapoiweka *hivi*, huh-uh. Na kwa hivyo sina budi kuirudisha nyuma kidogo.

³⁷ Nami nilikuwa nikimwambia Ndugu Neville kuhusu jambo hilo. Ndugu Neville akasema, "Ndiyo, lakini baada ya muda unaendelea kuisukumia mbali, unaisukuma mbali mpaka mkono wako usiwe mrefu kutosha kuifikia."

³⁸ Kwa hiyo, na—nashukuru kwa macho mazuri, hata hivyo. Na, sasa popote huko nje, jamani, ningeweza . . . Karibu naweza kuona unywele uliowekwa kwenye benchi kule chini, mahali fulani. Kwa hivyo, ni mazuri sana, kwa njia hiyo. Lakini nazeeka tu, hivyo tu.

³⁹ Kwa hiyo ninazidi kuzeeka hapa, lakini mdogo Huko, mnaona, na hiyo ndiyo sehemu yake nzuri. Kwa hiyo, siku fulani

tukufu, hata hivyo, Bwana Yesu atakuja, na yote tuliyokuwa tulipokuwa katika upeo wetu, tutakuwa tena, milele. Ila, mauti iliingia, kusababisha haya. Mauti iliingia, kuweka hizo mvi kichwani mwako. Mauti iliingia kuweka makunyanzi hayo usoni mwako. Lakini inaweza tu kukuchukua, hivyo tu. Kisha, katika kule kurudishwa, kile ulichokuwa katika upeo wako, kabla mauti haijakugusa kamwe, ulipokuwa na yapata miaka ishirini na mmoja, ishirini na miwili, hivyo ndivyo utakavyokuwa katika ule ufufuo. Ninaweza kuthibitisha hilo kwa Maandiko. Na hilo linatufanya tuwe na furaha sana, kujua jambo hilo. Hata iweje, haileti tofauti yoyote kwa vyovyote vile, kwa sababu tunarudi moja kwa moja tena, wapya, mara nyingine tena.

⁴⁰ Na, sasa, Kitabu cha Waebrania ni Kitabu ambacho tunaamini kwamba Paulo alikiandika. Hakuna—hakuna kumbukumbu ya kuonyesha kwamba kweli alikiandika. Lakini tunaamini ya kwamba Paulo aliandika Kitabu cha Waebrania, kwa sababu kilinini. . . kinasikika kama ni maandishi ya Paulo. Na karibu wanatheolojia wote wanaamini kwamba kiliandikwa na Paulo, pia. Lakini hata iwe ni nani, ni mwandishi yupi aliyekiandika, hakika ni kazi nzuri sana, na kimevuviwa, na kinashikamana na Biblia nzima.

⁴¹ Nacho kinaleta vivuli vyote. Na kwa kuwa, mimi mwenyewe, sijasoma, sina elimu, inanibidi kwa namna fulani kuchukua, na kujifanya mwainishaji, kusudi nijue ya kwamba ninayo Kweli ya Neno, kwa maana mimi daima huangalia nyuma katika Agano la Kale.

⁴² Sasa, kunao baadhi ya watu wanaoketi hapa, watatu ama wanne wao, ambao wamekuwa hapa tangu hili kanisa limekuwa hapa, nadhani, miaka ishirini na kitu, nilipotawazwa mara ya kwanza. Na kisha—kisha, wakati wote, nimejaribu kila wakati kufanya ninii. . . kuchunguza mifano.

⁴³ Kwa maneno mengine, kama sikuwahi kuliona jua, nami nikaona kile ambacho mwezi ulifanya, ukaitupa nuru duniani, na kadhalika namna hiyo, nao ukimulika kutoka mbinguni, ningekuwa na wazo fulani la vile jua lingekuwa litakapoanza kuwaka, kwa sababu ingekuwa. . . Nimeutazama mwezi; ni uakisi wa jua.

⁴⁴ Vema, mambo yote ya kale, ya Agano la Kale, chini ya torati, yalikuwa ni mfano tu, ama uakisi wa kile kilicho katika Injili. Kwa hiyo kama unajua Agano la Kale, unaweza kuwa na wazo zuri sana kile Agano Jipya lilicho, maana. . . Na sasa Paulo anatoa jambo lile lile hapa, katika Kitabu cha Waebrania. Anaonyesha jinsi Agano la Kale lilivyokuwa, katika mfano. Agano Jipya ni dhihirisho la huo mfano. Kila mtu anaamini hivyo, sivyo?

⁴⁵ Hivyo ndivyo ninavyoamini katika uponyaji wa Kiungu kwa dhati sana, kwa sababu kwamba katika Agano la Kale, uponyaji

wa Kiungu ulikuwako wakati huo. Na ikiwa . . . Tuna kitu bora zaidi. Ikiwa Agano la Kale lilitoa uponyaji wa Kiungu chini ya kitu hicho kidogo, na jambo pekee Agano Jipya lilicho ni—ni kitu cha juu zaidi sana, na bora zaidi, Agano Jipya lina nini katika uponyaji wa Kiungu? Loo, lina mengi zaidi, mnaona. Kwa maana, Agano Jipya ni “mambo bora zaidi,” asema Paulo hapa katika Waebrania. Agano la Kale lilitoa . . . Loo, lilikuwa ni sawa.

⁴⁶ Kama vile nikitoka hapa, kwenda kufanya jambo fulani hapa usiku, kusoma, au—au kufanya ibada huko nje, na, vema, ni ninii . . . au niende popote ninapoweza kusafiri, na ni usiku wa mbalamwezi. Huo ni mzuri sana. Ninathamini hilo. Lakini ikiwa mwezi unaweza kutoa huo, jua litafanya nini? Nalo lina nguvu. Li—linauzima tu mwezi, hivyo tu; mnaona, ka—kamwe haupo tena.

⁴⁷ Na kama ukiangalia, jua linapochomoza, sababu ya mwezi kutong’aa, ni kwa sababu mwezi na jua vinachanganyikana. Mwezi na jua ni mmoja. Je, ulijua hilo? Mwezi si kitu ila ko—kombora linaloning’inia angani. Nalo jua linaumulika, ukiakisi nuru yake duniani. Jua linaangaza kupitia kwenye mwezi, kwa mwezi, kuakisi. Mnaona? Wakati jua likiwa *huku* kote, linatupa nuru yake *hapa* juu ya mwezi, nao mwezi unaiakisia duniani. Kwa maneno mengine, jua na mwezi ni mume na mke. Au, ama, jua na mwezi ni Yesu na Kanisa. Wakati Yesu ameondoka, Yeye huangaza Nuru Yake kupitia kwa Kanisa. Mnaona? Kwa hiyo, ikiwa mwezi utatoa Nuru, Jua lingefanya nini?

⁴⁸ Na kama torati ilitoa nuru, kama torati ilitoa uponyaji, Injili itafanya nini? Mnaona? Loo, itakuwa na nguvu! Sivyo? Bila shaka, itakuwa. Ni lini wao . . . Angalieni, kama, angalieni, Yesu . . .

⁴⁹ Safarini, walipokuwa wakipitia nyikani, wana wa Israeli, walianza ku—kudharau na kulalamika dhidi ya Mungu na dhidi ya Musa, nao wakatenda dhambi. Ndipo nyoka wakaingia, wakaanza kuwachoma na kuwama. Na wanakufa, wala hakuna hata tiba yao ingewasaidia. Nao hao watu wakafa, kwa maelfu. Ndipo Mungu akafanya mfano wa Kristo. Alifanya ninii . . . alimwambia Musa atengeneze nyoka wa shaba na kumweka juu ya fimbo. Sasa, huo ulikuwa ni mfano wa Kristo, (hiyo ni kweli?), yule nyoka.

⁵⁰ Sasa mnaweza kushangaa, baadhi yenu watoto katika Injili, “Kwa nini nyoka amwakilishe Kristo?” Naam, kwa sababu nyoka, nyoka mwenyewe, alikuwa . . . aliwakilisha dhambi iliyokwishakuhukumiwa.

⁵¹ Mungu alimhukumu yule nyoka, katika bustani ya Edeni. Alichukua, akampa hukumu yake pale. Akaing’oa miguu yake kutoka kwake, na kumshusha kutoka katika umbo la mwanadamu, na kumweka kwenye—kwenye—kwenye

kiwango. . . Vema, hakuwa. . . Mnaona, hu—huyo nyoka, kwanza kabisa, hakuwa mtambaaji. Biblia ilisema, “Alikuwa ni mnyama, na mwerevu zaidi kuliko hayawani wote wa kondeni.” Alitembea kama mwanadamu, na kila kitu, “mwerevu kuliko wote.” Lakini ile laana ilimlaani, ikaondoa werevu wa—wa—wake, au u—urembo wake; na kumtupa ardhini, na kumweka juu ya tumbo lake, apate kutambaa.

⁵² Na sasa yule nyoka, juu ya mlingoti, aliwakilisha dhambi iliyokwishakuhukumiwa. Naye alitengenezwa kwa shaba. Sasa, shaba inawakilisha hukumu ya Kiungu, si hukumu ya duniani wala hukumu ya kiakili, bali hukumu ya Kiungu. Mnaona? Madhabahu ya shaba, ambayo. . . madhabahu, ambamo dhabihu ziliteketezwa, ilitengenezwa kwa shaba, “madhabahu ya shaba.” Nayo ina maana kwamba ilikuwa ni ya Kiungu. Hapo ndipo gharama ya Kiungu ilipolipiwa, kwa shaba. Naye Mu- . .

⁵³ Na, kwa mfano, Eliya, alipotoka, “Nazo mbi—mbingu zilikuwa kama shaba,” alisema. Hukumu ya Kiungu juu ya watu, kwa sababu walikuwa wamemwacha Mungu, katika siku za Ahabu. Ndipo Gehazi akapanda kwenda kuangalia, kuona jinsi mbingu zilivyokuwa. Naye akashuka, akasema, “Zinaonekana kama shaba.” Mnaona, hukumu ya Kiungu!

⁵⁴ Ufunuo 1, Yesu alionekana. . . Ama, Kanisa, hasa, la Bibiarusi wa Kristo, lilimwona amesimama katika vile Vinara Saba vya Taa vya Dhahabu, na miguu ilikuwa imetengenezwa kwa shaba. Ambapo, shaba ni hukumu ya Kiungu ya Kanisa, huko nje juu ya ulimwengu. Mnaona? Hukumu ya Kiungu!

⁵⁵ Yule nyoka, ile shaba, ikinena juu yake. Sasa angalieni. Iliinuliwa juu, na juu ya mlingoti, uliwakilisha msalaba. Sasa, mambo matatu, sasa angalieni. Iliinuliwa kwa kusudi gani? Kwamba wangesamehewa nyoka wao. . . au, wangesamehewa dhambi zao, na kuponywa kuumwa kwao na nyoka. Hiyo ni kweli? Na kila aliyemtazama, aliishi; aliyekataa kumtazama, alikufa. Sasa, huwezi kushughulika na dhambi kwa njia yoyote, huwezi kushughulika na dhambi kwa njia yoyote, bila kushughulika na uponyaji wa Kiungu. Huwezi kabisa kufanya hivyo. Hakuna njia ya kuihubiri Injili bila uponyaji wa Kiungu. Huwezi kulifanya. Hiyo ni kweli.

⁵⁶ Sasa angalieni hapa. Kwa mfano, kama hapa palikuwa na mwanamume, naye alikuwa amesimama hapa na alikuwa akinipiga tu kwa nguvu awezavyo, kwa ngumi yake. Vema, sasa, ili kumwondosha mtu huyo anayenipiga ngumi, hakuna haja kuukata mkono wake. Mnaona? Ama, labda ananipiga teke kwa mguu wake. Hakuna haja ya kuukata mguu wake. Sasa, jambo pekee la kufanya, ni kumwua mtu huyo, kutoka kichwani. Hiyo ni kweli? Ukikiua hicho kichwa, unaua mkono, unaua mguu. Na unaua mwi—mwili mzima (hiyo ni kweli?) ukimwua kutoka kichwani.

57 Vema, kichwa cha kiini hiki chote tulicho nacho hapa asubuhi ya leo ni nini? Kichwa cha hayo yote ni nini? Ni nini kilichosababisha magonjwa haya yote na dhambi na fedheha? Ilikuwa ni dhambi. Mnaona? Kabla ya kuwa na dhambi yoyote. . . Ugonjwa ni sifa, au kitu kinachofuata dhambi. Kama huna ninii. . . Kwa maneno mengine, ni kitu kinachotokana na dhambi. Mnaona? Kabla hakujakuwako na dhambi yoyote, hapakuwapo na ugonjwa wala chochote; hakuna wasiwasi, hakuna chochote; hakuna uzee, hakuna kulemewa, hakuna huzuni, hakuna nyumba zilizovunjika, hakuna chochote. Mnaona? Kulikuwa kukamilifu tu. Vema, kilichosababisha hayo, kilikuwa ni dhambi, d-h-a-m-b-i. Vema, basi, ugonjwa ukafuata dhambi. Nyumba zilizovunjika, sifa, maisha machafu, na mambo hayo yote, yalifuata dhambi.

58 Sasa, kama ukiua dhambi, huna budi kuziua sifa zake. Sivyo? Huwezi—huwezi kugusa. . . Huwezi kujipumbaza na dhambi, isipokuwa uwe unajipumbaza na hili. Na unapojipumbaza kwa hili, matokeo yake ni dhambi. Unaona? Sasa, kama ukiua dhambi, basi unaua kitu hicho chote.

59 Na sasa—sasa, unasema, ugonjwa, wakati mwingine unaugua, na kusema, “Je, nilitenda dhambi?” Loo, huenda isiwe ni wewe uliyetenda dhambi, lakini, kumbuka, magonjwa hupatiliza kufiki-. . . Maovu ya wazazi juu ya watoto, na watoto wa watoto, na watoto wao, hata kizazi cha tatu na cha nne. Mnaona? Na ni kudhoofika tu, kuchakaa, kwa miili ya wanadamu, huku dhambi ikilundikana, na kadhalika. Kama vile magonjwa ya zinaa, na kadhalika, yanaendelea kupatilizwa.

60 Hapa siku moja, daktari maarufu hapa, alikuwa na wasichana wawili ambao waliwaingiza ndani na kuwachunguza. Walikuwa wakipofuka. Nao wakagundua, ugonjwa wa zinaa. Wasichana wadogo safi na wenye maadili mema wawezavyo kuwa, papa hapa katika jiji hili, wote wawili wakiingia upofu. Nao hawakuja la kufanya. Wakatengenezewa miwani, nao mara moja wakaachana nayo. Ndipo wakawapima damu, na huo hapo. Nao wakachunguza tena; ilikuwa ni babu wa babu yao. Mnaona?

61 Haya basi, sasa. Mnaona, inashuka kupitia kwenye vizazi. Inavunjika. Vema, basi, unaposhughulika na dhambi, unashughulika na magonjwa, wakati uo huo.

62 Sasa, Musa alimwinua yule nyoka. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 3, “Kama Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa.” Je, hiyo ni kweli? Kwa maneno mengine, huo ulikuwa mwezi kwa jua. Ilikuwa ni kivuli cha kile kilichokuwa kinakuja. Vema, kama uponyaji wa Kiungu ulikuwa katika kumwinua yule nyoka wa shaba, hauna budi kuwa katika kumwinua Yesu Kristo. Kwa maana ilikuwa, kwa kuwa yote

aliyokuwa yule nyoka wa shaba, yalikuwa ni uakisi wa Yesu Kristo, katika dhambi iliyokwisha kuhukumiwa katika hukumu ya Kiungu, hukumu ya Kiungu ya Mungu. Sio hu- . . .

Ulimwengu ulimhukumu, na kumwua.

⁶³ Lakini hukumu ya Kiungu ya Mungu ilimfanya Mtu asiye na hatia, dhambi, amina, na—na kuihukumu pale pale. Mnaona? Naye aliibeba hukumu ye—yetu ya Kiungu, na kuichukua adhabu yangu, akichukua dhambi zako, na hatia yako, na tiketi yako ya kuzimu, na tiketi yako ya mateso. Na kujitwika Mwenyewe, na akafa badala yetu, na akapelekwa kuzimu badala yangu. Amina.

⁶⁴ Wala Mungu hakutaka Yeye abaki mle, bali alimfufua siku ya tatu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Kuangalia huko, na kusema, “Mimi ni . . . Mungu amenithibitishia kabisa, ya kuwa nimehesabiwa haki, kwa sababu alimfufua Mwanawe, Kristo Yesu. Kwa hiyo, nimefufuliwa pamoja Naye, nikiketi katika mahali pa Mbinguni.” Hiyo ni kweli. Alilitatua! Mnaona? Akahesabia haki. Alifufuka kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu.

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele;
Siku moja yuaja—loo, siku yenye utukufu!

Ndivyo ilivyo. Haya basi. Hapo ndipo:

Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu
chochote pungufu

Ya Damu ya Yesu na haki;

Wakati yote yanayoizunguka nafsi yangu
yakitoweka,

Yeye basi ndiye tumaini langu lote na nanga
yangu.

Kwa kuwa kwake Kristo, Mwamba wenye
imara, nasimama;

Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao,

Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

⁶⁵ Haya basi. Hapo ndipo matumaini yetu yanapotulia, papo hapo. Loo, jamani! Loo, ninapowazia jambo hilo, na kuwazia kule! Naye Yesu alisema, “Kama Musa alivyomwinua yule nyoka,” kusudi lile lile, jambo lile lile. “Kama vile tu Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa.”

⁶⁶ “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Sisi sote kama kondoo tumepotea; Mungu aliweka juu Yake maovu yetu sisi sote.” Haya basi. Loo, jamani! Nafikiri huko nyuma, Agano, wakati hao manabii wa Agano la Kale walipotazama mbele huko, katika ono, na kumwona

akipitia Yerusalemu akielekea Kalvari, akizibeba dhambi zetu kule msalabani. Na humo ndani akasema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu.” Wakati Isaya, alipopata tazamo la mara moja siku moja, na kusema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.”

⁶⁷ Unafikiri walikwenda wapi, walipoenda kwenye kaburi lao, wakiangalia mle? Si ajabu, Daudi alisema, “Mwili wangu utakaa katika matumaini. Kwa maana hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu, wala Yeye. . . Ama, hataiacha nafsi Yake katika kuzimu; wala hatamwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu. Kwa hivyo, kwa moyo wangu, ukapendezewa, na ulimi wangu ukafurahi.” Daudi aliuona huo katika kivuli, naye akashangilia. Kwa sababu, alijua, Kristo alipokufa, hilo lilitosha, kutoka Umilele hata Umilele. Amina. Yote yalikuwa yamekwisha basi.

⁶⁸ Isaya alisema kutakuwa na wakati ambapo kutakuwa na uponyaji. Ati kuzungumza juu ya uponyaji? Kasema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa kwake sisi tuliponywa.”

⁶⁹ Utaaliondoaje kwenye Maandiko? Huwezi kufanya hivyo, ndugu. Unaweza, unaweza kuligonga na kulipiga vita, na chochote kile, bali litaendelea moja kwa moja. Kupitia nyakati zisizo na mwisho na dahari, bado litaendelea.

⁷⁰ Paulo akizungumza hapa, ajabu sasa. Sehemu ya kwanza ya mlango huu wa 6, hebu turudi nyuma na kulitafakari kidogo. Sasa tutaanzia hapa, aya ya 12, ya 13, mahali fulani. Kupata tu msingi mdogo, baada ya Roho Mtakatifu kushuka sasa, na pamoja nasi, na kutulia juu yetu.

⁷¹ Sura ya 6 inazungumza sasa kuhusu dhambi isiyoweza kusamehewa. Tulipitia hayo yote hivi majuzi. Tulianza kwenye mlango wa 6, lakini tukaingia kwenye *Dhambi Isiyosameheka*. Ni wangapi hapa ndani wanaojua dhambi isiyosameheka ni nini sasa? Hakika. Kuukataa Ukweli wa Injili! Hiyo ni kweli? Kama. . .

⁷² “Atendaye dhambi kwa kusudi baada ya kupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi.” “Injili inapowekwa mbele zako, kwa uwazi,” Maandiko yanasema, “nawe unaiona; na kwa kuwa unataka kuwa tofauti, au kukubaliana na kundi hili; hata kwa makusudi unaiondokea; umemkufuru Roho Mtakatifu, na kamwe huwezi kusamehewa katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” Hiyo ni kweli.

⁷³ Wao walijua ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Nao wakasema. . . Walijua alikuwa.

⁷⁴ Nikodemo alilielezea. Akasema, “Mbona, hakika, tunajua Wewe u Mwalimu umetoka kwa Mungu.”

⁷⁵ Akasema, “Kwa sababu Yeye anasema... Ana ibilisi!” Wakati, maana, Yeye angeweza, angeweza kusimama pale na kuwatabiri; kwa sababu angeweza kuwatazama wasikilizaji na kuwaambia walichokuwa wakiwazia, akilini mwao; na angeweza kuwaponya wagonjwa, na kadhalika; awaombe, na kupata matokeo. Walisema, “Ah! Huyu ni ibilisi!”

⁷⁶ Naye akasema, “Sasa hebu kidogo. Mtasamehewa kwa ajili ya jambo hilo, kwa sababu mnanena dhidi Yangu. Lakini Roho Mtakatifu atakapokuja, msitoe tamshi kama hilo. Kwa—kwa maana, kumbukeni, Roho Mtakatifu atakuonya, moyoni mwako. Hakuna njia Kwake kufanya hivyo sasa, kwa maana ile chembe ya Damu niliyefungiwa bado haijavunjwa. Lakini siku moja, mkuki utaufungua ubavu huu, ndipo chembe ya Damu itakuwa wazi wakati huo. Nao Uhai Wangu utatoka, na kuingia ndani ya Baba, nao utarudi katika mfano wa Kiungu na nguvu. Ndipo ile chembe ya Damu itakuwa pale, naye Roho Mtakatifu atashughulika na kila moyo wa mwanadamu, kila mahali. Basi ukiikataa ile Kweli makusudi inapowakilishwa kwako, hakuna msamaha katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” Unaona, afadhali utembe kwa uangalifu. Haya basi. Unaona?

⁷⁷ “Kwa maana atendaye dhambi, ama kutokuamini, makusudi, baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena dhambi kwa ajili ya dhambi, bali kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto, ambao utamla yeye apingaye. Yeye aliyekidharau kile kivuli, chini ya torati ya Musa, alikufa pasipo huruma, kwa mashahidi wawili au watatu; ni adhabu kubwa zaidi jinsi gani, ingawa inastahili,” mhubiri, awe ni nani, “aliyeikanyaga Damu ya Yesu Kristo chini ya miguu yake, aliyelihasabu agano alilotakaswa kwalo,” kumbukeni, mtu aliyetakaswa, “kuwa ni kitu kiovu, na kuyafanya jeuri matendo ya neema. Mnaona, hakuna kitu kilichosalia kwake ila moto mkali, nao utamla yeye apingaye.”

⁷⁸ Wakati u—unapooni Kweli ya Injili, nawe unaikanyagia chini moja kwa moja; ili kuwa tu maarufu, ama kwenda kwenye kanisa lako mwenyewe, ama kuwa na njia yako mwenyewe kulihusu; ndugu, umefanya jambo fulani basi, ambalo, umekwisha. Hilo si neno langu sasa; ningependa kulifanya kitu tofauti. Lakini hivyo ndivyo Neno la Mungu linavyosema juu yake, sasa, Naye anashughulikia hilo.

⁷⁹ Sasa tunaanzia hapa kwenye kifungu cha 13, “Kwa kuwa wale ambao Mungu amewaahidi...” “Kwa maana Mungu alipokuwa ameahidi,” hasa.

... Mungu alipokwisha kumpa Ibrahimu ahadi, kwa sababu hakuna aliye mkuu kuliko yeye awezaye kumwapa, aliapa kwa nafsi yake,

⁸⁰ Mnaweza kuwazia tunaishi katika agano la jinsi gani! Sasa, kila... Hebu tusome tu mbele kidogo.

Akisema, Hakika kubariki nitakubariki, na kuzidisha nitakuzidisha.

Na hivyo, baada ya kuwa . . .

⁸¹ Kampa Ibrahimu ahadi hii, na akaahidi kwamba angeninii—angembariki na kumzidishia katika lolote atakalofanya.

⁸² Sasa tazama. Mungu pia, baada ya haya, alikula kiapo, akaapa kwamba atafanya hivyo. Sasa, Mungu aliapa kwa nafsi Yake, ya kwamba ataninii—kwamba atathibitisha kiapo ambacho alimwapia baba Ibrahimu.

⁸³ Basi alimthibitishia nini baba Ibrahimu? Alimwambia Ibrahimu, Yeye alimpa agano, bila masharti, si kwa sababu Ibrahimu alikuwa Ibrahimu. Tumepitia hilo, wiki chache zilizopita, mwajua. Alimpa Ibrahimu agano, kwa maana Mungu Mwenyewe alimteua Ibrahimu na kumchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ibrahimu, kabla hajapata kuzaliwa duniani, Mungu alijua yote kumhusu, alijua yale angefanya. Na, kwa neema, alimchagua Ibrahimu; wala si Ibrahimu pekee, bali Uzao wa Ibrahimu, baada yake. Loo, jamani! Kama ukininii . . .

⁸⁴ Jinsi tulivyo na msingi thabiti, kwamba, Mfalme wa wafalme wote, wakati Mungu wa miungu wote, wakati Mfalme wa wafalme wote, Bwana wa mabwana wote, Mwanzo wa mianzo yote, Mwenyewe, aliapa, kwa nafsi Yake, kwani ambapo hapana aliye mkuu zaidi, kwamba angethibitisha agano hili pamoja na Ibrahimu na kwa Uzao Wake!

⁸⁵ Sasa, loo, hili kidogo linaweza kwa namna fulani kung'oa, na kuvuta, na kusukumia nje, na kutoa nje, lakini hebu tuliangalie vizuri sana usoni tuone sura yake.

⁸⁶ Ikitulazimu, tunaweza kurudi nyuma na kuchukua agano la Ibrahimu, ambalo Mungu alifanya naye, na jinsi Mungu alivyoapa kwa nafsi Yake. Je, kuna mtu anayejua mahali ambapo Mungu aliwahi kuapa kwa nafsi Yake? Hebu tufungue sasa, Mwanzo mlango wa 22, naamini, na yapata 16. Hebu na tuangalie Mwanzo, mlango wa 22 na kifungu cha 16, nasi tunaona hapa ambapo Mungu aliapa kwa nafsi Ya—Yake. Vema, ninaamini ndiyo hii sasa, kama sijakosea, mahali papo hapo, 22:16. Naam, tazama, kifungu cha 15.

Malaiika wa BWANA akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni,

Akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu, asema BWANA, . . . kwa kuwa umetenda neno hili, wala hukunizulia . . . mwanao wa pekee:

Kwamba katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitakuzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni na kama mchanga . . . ulioko pwani ya bahari; na uzao wako utamiliki malango ya adui zao;

⁸⁷ Mungu aliapa kwa nafsi Yake. Haleluya! Ikiwa hiyo haimfanyi jamaa kujisikia kupiga mayowe, “Haleluya,” hakuna . . . umekufa. Kweli. Loo!

⁸⁸ Mungu alisema, “Ibrahimu, kwa sababu umefanya hili! Sio kile ambacho mtu mwingine atafanya, lakini kwa sababu umefanya hili! Kwa imani ulitembea, nami nimeheshimu kitu hicho hapo. Sio kuheshimu matendo tena; sitaliheshimu hili. Nitaheshimu imani. Na kwa sababu umetenda neno hili, bila kujua matokeo yangekuwaje, nimekuokoa. Nitaokoa uzao wako. Nitaapa kwa nafsi Yangu.” Amina. “Na Uzao wako utamiliki malango ya adui yao.” Amina. Hilo latosha, kwangu mimi. Hilo linaninii tu . . . Hayo, hayo ndiyo yote yanayopaswa kufanywa.

⁸⁹ Hapa, Paulo analichukua hapa tena, katika Waebrania, apate kurejea kwake. Loo, waliona jambo hilo katika Wagalatia, katika Waefeso, na kote kote, wakirejea kwake, ya kwamba msingi wetu ni imara. Amina. Sio kitu fulani cha uwongo, kitu fulani juu ya ushirikina fulani wa kipagani. Lakini ni BWANA ASEMA HIVI, kwa kiapo. Amina. Mungu alikula kiapo kwa nafsi Yake! Loo, jamani! Ni msingi imara jinsi gani, enyi watakatifu wa Bwana! Naam.

⁹⁰ Mapepo wanapokuja, nguvu zinapokuja, magonjwa yanapokuja, kifo chenyewe kinapokukodolea macho usoni, kinapoteza tu mahali pake; kinayeyuka tu kama theluji kwenye nuru ya jua, tunapokitupa katika Nuru ya Injili pale.

⁹¹ Ukiangalia, watu, wakati mwingine unachukua . . . Mara nyingi sana, watu wakiandika kila namna ya vitu na kadhalika, inawatoa katika kanisa la Protestanti wakaingia kanisa Katoliki, kwa sababu Wakatoliki wanaamini Neno limevuviwa. Wanaamini hivyo. Wanaamini kwamba Marko 16 imevuviwa. Kabisa. Wanasema imevuviwa. Lakini, mnaona, ibilisi hufanya kazi katika jambo hilo, wanasema, “Kanisa liko juu ya Neno.”

⁹² Vema, basi, Mprotestanti anakuja, anaona kitu ambacho haninii . . . kitu kidogo cha kale ambacho hawakubali, hakubaliani nacho. Vema, anasema, “*Hii* haijavuviwa. *Hii* ni tafsiri mbaya ya Neno.” Akijaribu tu kuleta athari, mnaona, kushikilia, ama kuingiza theolojia yake fulani maalum. Mnaona? Hilo halina uhusiano wowote Nalo.

⁹³ Hilo ni Neno la Mungu. Ninaamini kila Neno Lake. Ni . . . si kazi yangu kuondosha *hili*, kuondosha *lile*. Jukumu langu ni kuishi kulingana na maagizo Yake, hivyo tu, mpaka mahitaji Yake, hasa, ikinibidi kuliishia Hilo. Kwa maana Mungu ameapa, na akasema, “Yule ambaye ataongeza chochote Kwake au kuondoa chochote Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake, ya Kitabu cha Uzima.” Hiyo ni kweli? Kwa hiyo, tunaamini Hilo.

⁹⁴ Ikiwa msingi wetu ni thabiti na ni wa hakika, katika Yesu Kristo, basi, ndugu, hakuna kitu kinachoweza kukutikisa. Unaninii tu . . . Umetiwa nanga. Amina. Loo, aisee! Vema.

95 “Na baada ya . . .” Ki—kifungu cha 15 sasa.

Na hivyo, kwa—kwa kuvumilia, akaipata ile ahadi.

96 Loo, tuseme, sijui kama tutashuka kwenye mlango huo wa 7, ama la.

. . . baada ya kustahimili (amina), aliipata ile ahadi.

97 Unaweza kufanya jambo lile lile, asubuhi ya leo? Unaweza kuweka imani yako, na kusema, “Ni BWANA ASEMA HIVI?” Na haijalishi kijacho wala kiendacho, iwe rahisi leo, kesho iwe ngumu, kesho yake wanakuchokoza, kesho yake wanakudhihaki, kesho yake wanasema mimi ni “mwenye kichaa,” navumilia. Amina!

98 “Baada ya!” Sio *kabla* ya kustahimili, lakini, “Baada ya kustahimili, alipata ile ahadi.” Amina. Loo, jamani! Hiyo hapo. Mnaiona? Ndugu, hilo hutikisa na kuondolea mbali pepo wote na chochote kile. Mnaona? Mnaona? Hiyo hapo.

99 Ndipo Shetani akaja, akasema, “Loo, sasa, nakwambia, umesisimkwa kidogo. Afadhali ki—ki—kidogo tu utumie akili kuhusu jambo hili.”

Sema, “Ni BWANA ASEMA HIVI, Shetani!”

100 Haijalishi inakuwa ngumu kiasi gani, jinsi inavyoonekana, yale mtu yeyote asemayo! “Ninataka kufanya hivyo; kwa subira.” Sio kuhangaika! Mtu hawezi kuwa na subira, huku anahangaika kila wakati. Inakubidi tu kuweka matanga yako moja kwa moja pale, na kuendelea moja kwa moja. Haijalishi nini kinatokea; endelea moja kwa moja.

101 Sikilizeni. Nitasema kitu fulani. Angalieni. Imani haina fahamu. Amina. Mnaamini hivyo? Nimejifunza hilo katika miaka ya kusafiri kote duniani, na kukutana na watu wa matabaka mbalimbali. Lakini, imani haina fahamu. Una imani na hata hujui. Hiyo ni kweli.

102 Yesu Kristo, haidhuru, kama alikuwa katika dhoruba na tufani inaipiga mashua kutoka upande mmoja hadi mwingine, au alikuwa amesimama usoni, lundo la pepo; kama alikuwa amening’inia mahali popote, haikumtikisa kamwe. Aliendelea moja kwa moja, mtulivu na mnyamavu alivyoweza kuwa. Kwa nini? Hakuwa na fahamu ya woga au kitu chochote kilichomzunguka. Hiyo ni kweli. Kama ingetukia, au kama haingetukia; Alijua ingetukia kwa sababu Mungu alisema hivyo. Yeye hakusema, “Ee, nimeomba vya kutosha? Sijui kama nilifunga kwa muda mrefu kutosha? Sijui kama nilifanya *hivi*?” Aliendelea mbele tu, bila fahamu. Hiyo ni kweli. Aliamini yale aliyosema Mungu ni Kweli. Hayo maneno hayana budi kutimizwa, Naye alijua maisha Yake yalikuwa nini kuyatimiza. Hiyo ni kweli.

103 Nawe uko hapa kulitimiza, pia. Tembea tu bila fahamu ya hofu. Tembea bila fahamu ya ukosoaji. Tembea ulimwenguni bila

fahamu. Tembea, unapotembea katika Kristo, tembea pamoja Naye. Pasipo kuzingatia, mkono wa kulia au wa kushoto; endelea tu. Kama jambo fulani likiibuka kanisani; tembea pamoja na Mungu. Haleluya! Ugonjwa ukikupata; tembea pamoja na Mungu. Ikiwa jirani hakupendi; tembea pamoja na Mungu. Endelea tu kutembea pamoja na Mungu.

¹⁰⁴ Henoko, siku moja, alitembea namna hiyo. Mnajua alichofanya? Alitembea kote kote hata Nyumbani, pamoja na Mungu; alifika mbali sana njiani, hakutaka kurudi tena. Amina.

¹⁰⁵ Tembea pamoja na Mungu! Daktari anasema utakufa; tembea na Mungu. Naam. Daktari anasema huwezi... Vema, tembea na Mungu. Tembea tu na Mungu, hivyo tu. Kwa maana Mungu amekuahidi, "Sitakuacha wala sitakupungukia kamwe. Nitakuwa pamoja nawe hata ukamilifu wa dahari." Naye akaapa, kwa lile agano alilokupa, ya kwamba atalithibitisha. Tembea tu na Mungu, basi.

¹⁰⁶ Utakuwa na heri na shari zako. Usijali. Huna budi kupitia sehemu zenye miiba, juu ya mawe yenye ncha kali, kupanda miinuko mikali, kushuka mbavuni mwa vilima, kupanda kupitia milimani, juu ya maji; lakini tembea na Mungu. Naam, bwana. "Kuna vilima vingi sana vya kupanda, kuelekea juu," umesikia ule wimbo wa kale, "lakini jinsi yatakavyoonekana ni madogo utakapofika mwisho wa safari." Jamani, jamani! Angalia tu kule, yote ambayo yamekuwa, angalia nyuma kwenye nyayo za miguu yako; hayatakuwa mengi sana.

. . . baada ya . . . kuvumilia, aliipata ile ahadi.

Watu, maana wanadamu . . . huapa kwa aliye mkuu kuliko wao: na kiapo cha . . . kinathibitishwa, ukomo wa mashindano yote ni kiapo, kwa kuyathibitisha.

¹⁰⁷ Kwa maneno mengine, watu wanapoapa, wakija kwenu na kula kiapo, ndio mwisho wa mashindano yote; unaamini, unaona.

Katika neno hilo Mungu—katika neno hilo Mungu akipenda zaidi, loo, akipenda zaidi kuwaonyesha zaidi sana warithio ile ahadi, jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, loo, aliithibitisha kwa kiapo:

¹⁰⁸ Mungu alitaka kukuonyesha. Kwa shauri Lake, alitaka. Aliithibitisha kwa kiapo, ya kwamba nyinyi hamtakuwa na mashaka juu yake. Sasa tazama hapa.

Ili kwa vitu viwili visi-. . . vitu—vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo Mungu hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kwa . . . kuyashika matumaini yake yawekwayo mbele yetu:

109 Haiwezekani kabisa kwa Mungu kusema uongo. Hilo ni jambo moja. Hiyo ni kweli? Sasa, haiwezekani kwa Mungu kusema uongo. Kuna mambo mawili. Kwanza, haiwezekani kwa Mungu kusema uongo. Sasa, jambo la pili ni, kwamba Mungu Mwenyewe, ambaye hawezi kusema uongo. . . Ili kuikamilisha, maradufu, aliapia, amina, kwamba angethibitisha kiapo hiki. Loo, ninii kuu jinsi. . .

110 Hebu turudi nyuma tuone kwamba kiapo ni nini. Je, mtaweza, kidogo, kidogo tu? Nyuma katika—katika Kitabu cha Mwanzo, nilikuwa nikiusoma hapa hivi majuzi, mlango wa 15 wa Mwanzo. Huu hapa basi. Sikilizeni kiapo ambacho Mungu aliapa, ukitaka kusoma kitu cha kukufanya ujisikie vizuri kweli.

Baada ya mambo hayo neno la BWANA likamjia Ibrahimu katika njozi, likisema, Usiogope, Ibrahimu: Mimi ni ngao yako, na. . . thawabu yako kubwa sana.

111 “Mimi ni ngao yako.” Ikiwa Mungu ni ngao yako, ibilisi atakupigaje? Unaona? Unaona? “Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana.” Ni nani? “Mimi,” Bwana, “thawabu yako kubwa sana.”

Ibrahimu akasema, Bwana MUNGU, utanipa nini, nami naenda zangu hali sina mtoto, na atakayemiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri Mdamaski?

Naye Ibrahimu akasema. . .

Abramu akasema, Tazama, hukunipa uzao, na, tazama, mtu aliyezaliwa nyumbani mwangu ndiye mrithi wangu.

Na, tazama, neno la BWANA likamjia, likinena, Huyu hatakurithi; bali yeye ajaye. . . atakayetoka katika viuno vyako ndiye atakayekurithi.

112 Mungu tayari alikuwa amemwambia, miaka ishirini na mitano awali, ya kwamba atafanya hivyo. Kwa hiyo Ibrahimu akaanza kushangaa sasa, “Sasa, Bwana, wapi, itatendekaje sasa? Na, unaona, nina umri wa miaka mia moja.”

113 Sasa angalieni, “Naye akamtoa nje. . .” Hapa, inakuja.

Akamleta nje, akasema, “Tazama sasa kuelekea mbinguni, kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu: akamuambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.

114 Na hata hivyo hata hakuwa na watoto, na umri wa miaka mia moja. Kasema, “Tazama mbinguni. Je, unaweza kuzihesabu hizo nyota?”

115 Na hapa, kule Mlima Palomar, ama Mlima Wilson, hasa, huko California, nikiangalia huko nje kwenye chumba hicho kikubwa cha kuchungulia, ambako unaweza kuchukua darubini na kuona miaka milioni mia moja na ishirini ya anga la nuru. Sasa, unafikiri, macho yako yanaweza kuona umbali wa maili

elfu kadhaa tu, unaona, labda milioni kadhaa, milioni chache. Lakini hii ni miaka milioni mia moja na ishirini. Angalia tu, unaweza kuona kwenye mfumo wa jua, nyota tupu tu. Baadhi yazo ziko karibu zaidi, na baadhi yazo ziko mbali zaidi, na kadhalika. Lakini ukiangalia miaka milioni mia moja na ishirini ya anga la nuru, wazia tu ni nini, jinsi nuru inavyosafiri kwa kasi. Na miaka milioni mia moja na ishirini ya anga la nuru, mbona, usingeweza kuandika safu za takwimu zake kuzunguka kanisa hili, mara kumi, za tisa, uone itakuwa ni maili ngapi. Na huko nje, bado kuna miezi na nyota, nje ya hapo.

¹¹⁶ Uzao wa Ibrahimu! Kisha, ati uzihesabu? Usingeweza kuzihesabu. “Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.” Basi sikilizeni. Hiki hapo kilichofanya hivyo.

Akamwamini BWANA; loo, naye akahesabiwa jambo hili kuwa haki.

¹¹⁷ Kamwe hakusema, “Sasa, Bwana, nitakuambia nitakalofanya. Nitafanya jambo *fulani-fulani*. Nami nitafanya *hili*, au *lile*.” Yeye, yeye alimwamini tu Bwana, naye akahesabiwa jambo hili kuwa haki, maana Mungu alisema hivyo. Alikuwa ameapa kwa jambo hilo, ya kwamba angelitenda.

Kisha akamwambia, Mimi ndimi BWANA niliyekuleta kutoka Uru wa...Kaldayo, nikupe wewe nchi hii ili urithi.

Akasema, Ee, Bwana MUNGU, nipateje kujua kwamba nitairithi.

¹¹⁸ “Sasa, sina watoto sasa. Lakini je, unaweza kunipa namna fulani ya ishara?”

¹¹⁹ Unajua, mimi si mtafuta-ishara, lakini ninaamini katika ishara. Hiyo ni kweli. Mnaona? Ikiwa hakuna ishara isiyoonekana iliyotolewa kwa watu, siku hizi. . .

¹²⁰ Mbona, si ajabu watu hawawezi kuamini! Wanazunguka huku na huko, nao watu waliiondoa tu mambo yote ya kimbinguni kutoka katika Biblia, na wakachukua tu. . . Sasa, m—mtu anakuja na kusema, “Nimeokoka.” Hakika. Naam, huwezi—huwezi kumshuku. Hiyo ni kweli. Huwezi kumshuku. Mtu huyo anajitokeza barabarani, mlevi tu awezavyo kuwa, na—na sigara kinywani mwake, huku anayumbayumba, akipiga kelele “whoopii,” na kulaani, kila apumuapo. Angeweza kusema, “Nimeokoka, kwa sababu ninaamini.” Huwezi. . . Utasema nini juu yake? Hakuna uwezacho kufanya. “Kanisa langu linanikaribisha. Mimi ni mfuasi wake.” Utafanya nini kuhusu hilo? Hakuna unachoweza kufanya. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

¹²¹ Lakini njia pekee unayoweza kujua ni kwa ishara. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli kabisa. Inabidi uone ishara, ili kulionyesha. Sasa, kama ni imani pekee, basi imani haifanyi hivyo.

¹²² Ibrahimu alimwamini Mungu, hiyo ni kweli, naye akahesabiwa jambo hili kuwa haki. Lakini Mungu alimpa ishara; akamtahiri, kama ishara, muhuri. Basi, uzao wa Ibrahimu bado unapokea tohara. Walifanya hivyo kote katika wakati, mpaka mwe—mwezi ukafifia, torati, naye Mwana akaingia. Basi Mwana wa Mungu alipokuja, Yeye bado aliwatahiri.

¹²³ Na kila mwana wa Ibrahimu anatahiriwa siku hizi, si kwa mwili, na kwa moyo. Roho Mtakatifu huutahiri moyo, anakatilia mbali mambo ya ulimwengu, na kukufanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. *Tohara* ni “kukatilia mbali nyama ya ziada.” Wanaume tu ndio wanguweza kutahiriwa. Wanaume wote walikuwa ndio pekee waliokuwa katika hilo agano. Naye mwanamke, akiwa ameolewa, akaingizwa ndani. Hebu chukua, siku hizi, ikiwa . . . Sasa sisemi . . .

¹²⁴ Kuna wanawake wengi hapa, na wanawake ni watu wazuri sana. Kama Mungu angaliweza kumpa mwanamume kitu chochote kilicho bora zaidi kuliko mwanamke, angefanya hivyo. Lakini alimpa mwanamke.

¹²⁵ Lakini huu ni ulimwengu wa mwanamke. Yeye anaendesha kitu hicho chote. Si nyinyi mama wa nyumbani hapa; lakini ninamaanisha huko nje ulimwenguni. Hebu tuseme, acha maskini mvua nguo mmoja huko Hollywood, aanze kukata nywele zake, baadhi ya wanawake, angalia wasichana wote wakikata nywele zao kwa njia ile ile. Ama, waanzishe mtindo fulani, katika mavazi, kisha uwaangalie wasichana wote wakifanya jambo lile lile; Wakristo na wote, wanavyojiita. Hiyo ni kweli. Ni ulimwengu wa mwanamke.

¹²⁶ Mnaona, wanachora picha za—za malaika mwanamke. Hakuna kitu kama hicho. Nionyeshe mahali pamoja katika Maandiko. Kila Malaika ni mwanaume, si wanawake. Ati malaika wanawake, mama Mariamu, na mambo haya yote namna hiyo, hakuna kitu kama hicho. Tafuta sehemu moja katika Maandiko ambapo iliwahi kusema kulikuwa na Malaika mwanamke. Siku zote ni, “Wa kiume.” Mikaeli! Gabrieli! “Akachomoa upanga Wake.” Siku zote ni, “Mwanamume, Mwanamume, Mwanamume.” Hiyo ni kweli.

¹²⁷ “Mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwanamume, sio mwanamume kwa ajili ya wanawake.” Hakika. Lakini wao, jinsi wao . . .

¹²⁸ Huyu ndiye tu ibilisi alimchukua, mwanamke, katika bustani ya Edeni, awe chombo chake. Bado anamtumia. Hiyo ni kweli.

¹²⁹ Si walioongoka, si walioongoka! Mwanamke ambaye ni Mkristo, na mwanamke mwema, ndicho kitu bora zaidi ambacho mwanamume angeweza kupata, nje ya wokovu. Lakini yeye

asiye mzuri, ndicho kitu kibaya zaidi angaliweza kupata, huko nje. Hiyo ni kweli.

¹³⁰ Sulemani alisema, kwamba, “Mwanamke mzuri alikuwa kito katika taji ya mwanamume, lakini asiye haki alikuwa ni maji damuni mwake.” Damu yake ni uhai wake. Basi angekuwa na nini zaidi kuliko maji damuni mwake? Ingemwua.

¹³¹ Sasa angalieni, Mungu akinena na Ibrahimu. Sasa angalieni.

Akasema, Ee, Bwana MUNGU, nipateje kujua kwamba nitairithi?

Akamwambia, Unipatie ndama wa miaka mitatu, na mbu—mbuzi jike wa miaka mitatu, na kondoo dume wa miaka mitatu, na hua wawili, na mwana njiwa.

¹³² Hii hapa inakwenda. Itazame sasa.

Akampatia hao wote, akawapasua vipande viwili, akaweka kila kipande kuelekea mwenzake: . . . (Loo, jamani, ni—ni maana ya jinsi gani hawa waliyo nayo!) . . . lakini ndege hakuwagawa.

¹³³ Basi akampasua ndama na mbuzi, na kadhalika, vipande, na kuweka hivyo vipande, kipande kimoja kumwelekea mwenzake, ikionyesha kwamba vingeamana kutoka kipindi kimoja cha wakati hadi kingine. Lakini hua, na kadhalika, hakuwapasua.

Na ndege wa angani walipotua juu ya mizoga, Ibrahimu akawafukuza.

Na jua lilipokuwa likichwa, usingizi mzito ulimshika Abramu; na, tazama, hofu ya giza kuu ikamwangukia.

Akamwambia Abramu, Ujue hakika ya kwamba uzao wako utakuwa . . . mgeni katika nchi isiyo yake, nao watawatumikia watu wale; nao watawatesa, muda wa miaka mia nne:

¹³⁴ Mungu akitabiri, kwa Ibrahimu, kwamba chini kabisa katika vitukuu vya vitukuu vya vitukuu vyake wangekaa ugenini, miaka mia nne, watateswa. Muda uliteuliwa, hasa, kwamba ungekuwa muda gani. Sasa angalieni.

Hata na taifa lile watakaowatumikia nitawahukumu: na baadaye watatoka na mali nyingi.

¹³⁵ Walifanya hivyo. “Nawe utaninii . . .” Angalieni. Ninazungunza juu ya ninii takatifu . . . Angalieni. Na hata sio . . . Bila masharti! Ati nini?

Lakini wewe utakwenda kwa baba zako kwa amani; . . . (Amina!)

. . . utakwenda kwa baba zako kwa amani; nawe utazikwa katika uzee mwema.

¹³⁶ Siyo, “Ikiwa utafanya mambo fulani.” Lakini, “Tayari nimeshaifanya, nimetia alama.” Amina! Loo, jamani!

Ninasisimkwa kabisa, ninapopata jambo hili, mpaka mishipa yangu inaruka juu-na-chini mwilini mwangu, inavyoonekana. Ninapowazia juu ya ahadi hiyo, loo, ndugu!

¹³⁷ Nilikuwa nikimwambia mke wangu asubuhi ya leo. Nilitazama, nikasema, “Mpenzi, unajua . . .” Nilikuwa nikizungumzia juu ya ndu—ndugu yangu na hao, jinsi ambavyo wa—watoto wao . . . Huyu hapa Rebekah, anakaribia kuwa kijana mwanamke. Na—nami nikasema, “Ninataka kujaribu kuondoka hapa, kabla haijamlazimu kujiunga na shule hii, na kadhalika,” na kuendelea namna hiyo. Nami nikasema, “Unajua, sisi si watoto tena.” Nikasema, “Si mtoto mimi, kwa vyovyote vile.” Nikasema, “Unajua, nitakuwa na umri wa miaka arobaini na sita hivi karibuni.” Nikasema, “Ni—ninakuwa mzee.”

¹³⁸ Lakini, loo, jamani, basi wakati mawazo yangu yanapoangukia hapa kwenye kiapo cha Mungu nilichoahidiwa mimi, basi hayo yote yanatoweka tu basi. Ninanini tu . . . Kila kitu kinaonekana tofauti. Sasa angalieni, “. . .katika uzee mwema.”

Lakini kizazi cha nne kitarudi hapa, kwa maana uovu wa Waamori haujatimia bado.

¹³⁹ Mungu, akifanya ahadi Yake. Mungu alimpa Ibrahimu, bila masharti. Sasa angalia, wakati Yeye aliposema jambo hili. Loo, hii hapa picha nzuri, kama tungeweza tu kuwa na wakati wa kuimaliza, kabla hatujashuka kuimalizia hii, picha ambayo Mungu alikuwa ameitengeneza. Angalieni.

Akasema, “Nenda kaniletee ndama wa miaka mitatu.”

¹⁴⁰ Tazama, “tatu.” Kila kitu katika Biblia ni tatu. Tatu huunganika kuwa moja. Mnaona? Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; sio Miungu watatu. Mmoja! Imani, tumaini, na upendo; sio vitu vitatu mbalimbali, lakini yote ni kiini cha kimoja: upendo.

¹⁴¹ Sasa, basi, kulikuwa na kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; si vipindi vitatu mbalimbali vya nyakati, si kazi tatu za neema, bali kazi moja katika madhihirisho mbalimbali. Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa pamoja na Luther, chini ya kuhesabiwa haki; alikuwa chini ya Wesley, pamoja na utakaso; katika Kanisa sasa, katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu yeye yule! Si Roho Mtakatifu wawili; Roho Mtakatifu yeye yule!

¹⁴² Punje ndogo iliyochipuka hapa juu, katika kitu cha kwanza, naye mkulima akaangalia na kuona haya machipukizi madogo yakijitokeza. “Ajabu!” Alishangilia. Baada ya muda, yalizeeka na kunyauka, nayo mahindi yake yakaendelea. Ndani yake, uhai ule ule uliokuwa kwenye punje hii, hapa chini kwenye ubua wa kwanza, uko ndani yake hapa juu kwenye suke na punje, vile vile tu. Uliendelea tu, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea.

143 Ndivyo Kanisa linavyoendelea kukua, hadi Siku ile kamilifu wakati Yesu atakapokuja. Mnaona? Roho Mtakatifu yeye yule, jambo lile lile, kipindi tofauti tu cha wakati.

144 Sasa, katika kuendeleza Hili, angalieni. Wachukue ndama, mbuzi, na kila kitu, lazima wawe na umri wa miaka mitatu. Vipindi vitatu mbalimbali vya wakati; ubaba, uwana, Roho Mtakatifu. Mnaona? “Miaka mitatu,” kila kitu kilikuwa ni cha miaka mitatu; ilimaanisha, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Mungu yeye yule aliyekuwa chini ya kipindi *hicho* cha wakati, yuko chini ya kipindi *hiki* cha wakati, chini ya kipindi *kile* cha wakati, na atakuwa yeye yule. Mungu mmoja tu; vipindi vitatu vya wakati. Si Miungu watatu; vipindi vitatu vya wakati wa Mungu yeye yule!

145 Mungu yeye yule, aliyekuwa katika Nguzo ya Moto, alikuwa ndani ya Kristo Yesu. Yeye Yule, katika Kristo Yesu, ndani yako. Hiyo ni kweli. “Mungu ndani yako, tumaini la Utukufu.” Hiyo ni kweli? Ubatizo wa Roho Mtakatifu ukiishi ndani ya mtu sasa, mnafanyika (kitu gani?) wana wa Mungu.

146 Wakati Mungu alipojdhili, akamtia uvuli bikira Mariamu, Yeye alikuwa ni Uzima. Nao Uhai ukajifanya uvuli na kuumba chembe ya Damu kujizungushia Yenyewe.

147 Mtu yeyote anajua, sasa, ya kwamba chembe chembe ya damu inatoka (kwa kitu gani?) mume. Hiyo ni kweli? Uhai unakaa katika chembe ya damu, nayo hiyo chembe ya damu inatoka kwa mwanamume, sio mwanamke. Na hapo ndipo uhai ulipo, ni katika mbegu za mwanamume.

148 Angalieni, ndipo basi Mungu Mwenyewe akaingia katika tumbo la uzazi la bikira Mariamu, na kujifunika Mwenyewe katika chembe ya Damu iliyoubwa. Haleluya!

149 Hiyo ndiyo sababu tunao Uzima wa Milele. Ndipo wakati chembe hiyo ya Damu, kwa sababu ya dhambi, ilipochomwa kwa upanga kule, nayo ikavunjika, ilimwachilia Mungu kule. Nayo ikavunjika na kufungua chembe ya Damu na kutuoshia, na kutuleta ndani Yake Mwenyewe, kwa Roho Mtakatifu. Haya basi. Na sasa sisi ni wana wa Mungu, sehemu ya Mungu. Uungu Wenyewe unaishi ndani ya kila mwaminio. Kila mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu ni sehemu ya Mungu.

150 Si ajabu anaamini katika mambo ya Kimbinguni! Si ajabu anaweza kuamini chochote! Kwa nini hivyo? Ndani yake mna sehemu ya Mungu, iliyofunikwa katika mwili huo hapo unaopatikana na mauti; ambapo pana dhambi na kadhalika, ameumba mwili huu. Lakini huko chini, kazi ya Mungu pekee, katika kuzaliwa upya, imeshuka kupitia pale; kwa kumwagwa kwa Damu Yake Mwenyewe, na kuiondoa ile damu iliyokuwa mle ndani, kama njia, na kuiweka kando, na kuingia ndani ya mtu huyu mwenye dhambi. Na kuweka ndani yake tumaini

ya kwamba angekufa kwa ajili Yake, na huru kama vile angesimama pale. Aseme naye; hakika, analiamini!

¹⁵¹ Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: kwa Jina Langu watatoa pepo; na kunena kwa lugha mpya; watashika nyoka; au kunywa vitu; au wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Yesu alisema hivyo.

¹⁵² Kwa nini? Amekuwa sehemu Yake. Naam, bwana. Mungu yuko chonjo. Atawasilisha chochote. Atafanya njia. Wakati hakuna njia, Yeye hufanya njia. Na mtu yeyote anayemwamini, anaamini jambo lile lile. Hana budi kuamini. Yeye ni sehemu ya Mungu. Yeye ni mzao wa Mungu. Yeye ni mwana wa Mungu, ama binti wa Mungu. Wala hawezi kufanya lingine lolote, kwa sababu Mungu yuko pamoja naye. Yeye ni sehemu tu ya Mungu.

¹⁵³ Tazama. Kila kitu ambacho Mungu alikuwa, katika Nguzo ya Moto, alikimwaga ndani ya Mwana, Yesu Kristo. “Ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.” Je, hiyo ni kweli? Biblia ilisema hivyo. Mungu, M-u-n-g-u, Mwenyewe, Yehova, Mwenye Nguvu, Kinga, Ngao, majina Yake yote ya ukombozi, kila kitu alichokuwa, alikimwaga ndani ya Yesu Kristo.

¹⁵⁴ Naye Yesu Kristo, aliyezaliwa kutokana na chembe ya Damu. Basi kifuniko cha nje cha hiyo chembe, yenyewe, ambayo ni mabilioni mara mabilioni ndogo zaidi kuliko jicho la mwanadamu linavyoweza kuona, bali huo ulikuwa ni mwili, Bwana Yesu. Humo ndani mlikuwamo na Mungu Mwenyewe. Alijifunga Mwenyewe kwenye seli ya Damu, apate kuchukua Damu Yake Mwenyewe na kumwaga Damu Yake Mwenyewe, ama—ama kuitoa bure; ili kwamba sisi, kwa kupasuliwa kwa chembe hiyo ya Damu, kwetu tunaopatikana na mauti, wakati itakapovunjika, nao uhai wetu unaondoka kutoka hapa kwenda nje. Kupitia ukombozi, wa—wa Damu ambayo Mungu alihitaji, tunaweza kuingizwa katika Mwili huo na kuwa sehemu ya Mungu Mwenyewe, kama mwana wa Mungu.

¹⁵⁵ Ndugu, ukiweza kulimeng’anya Hilo, hakika litakufaa. Laiti ningalikuwa na njia ya ku—kuwaonyesheni tu kwamba ni nini. Hebu wazienu tu juu ya Mungu, Yehova, akishuka ndani ya tumbo la uzazi la mwanamke, akamtia uvuli. Akashuka katika ninii, sasa, Roho, Naye yuko mle ndani. Yeye ni nani? Yeye ni Muumba, Mwenyewe. Alimfanya mwanamke yuyo huyo na—na tumbo la uzazi alimokuwemo wakati uo huo. Mungu alijifanya Mwenyewe mdogo, akashuka na kuingia kwenye seli hii ya Damu. Naye akaanza kujenga kitu fulani kujizungushia. Ilikuwa ni nini?

¹⁵⁶ Mnaona, ja—jambo hili lilisababishwa na nini hapo mwanzo? Damu. Damu, uhai ulikuwa katika damu. Na huko nyuma ndiyo iliyosababisha hilo, hapo mwanzo. Sasa, ili kuliondoa, Mungu Mwenyewe hana budi kushuka.

157 Naye alijifanya kuwa mdogo sana. Akaingia katika tumbo la uzazi la Mariamu, na akajiambia Mwenyewe, ukuta, ambao ulikuwa ni chembe ya Damu; hamna mtu, la, hakuna kitu kuhusu Hilo. Aliumba seli hii ya Damu. Chembe hiyo ya Damu ikasukuma nyingine, nyingine, nyingine, na mishipa yote na kila kitu kikaanza kuingia. Naye Mungu, Mwenyewe, akiishia hii, akijenga maskani, Naye akakaa ndani ya Kristo.

158 Huyu hapo Mungu, akitembea-tembea. Akasema, “Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu yu ndani Yangu.”

159 Kasema, “Utuonyeshe sasa Baba.” Filipino akasema, “Unionyeshe Baba na yatanitoshia.”

160 Kasema, “Filipo, nimekuwapo pamoja nanyi muda mrefu sana, nawe hunijui?” Akasema, “Mnaponiona Mimi, mnamwona Baba. Basi kwa nini kusema, ‘Unionyeshe Baba?’ Mimi na Baba ni Mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu sasa. Si Mimi ninayetenda hizo kazi; ni Yeye aishiye ndani Yangu, ndiye anayetenda hizo kazi.” Loo, jamani!

161 Ningewezaje kumwambia mtu tatizo lake? Ningewezaje kumwambia maisha yake ya baadaye yatakuwaje, miaka kumi, ama alivyokuwa miaka arobaini iliyopita? Sio mimi. Haleluya! Yeye Ndiye anayeishi ndani yangu. Ambaye alishuka na, kupitia kwa Damu Yake, akanileta katika ushirika pamoja Naye. Haleluya! Mikono yangu ingewezaje kufanya lolote, kwa kuwaponya wagonjwa? Haina nguvu hata kidogo. Sio mimi. Lakini ni Yeye, anayeishi hapa ndani, ndiye anayazitenda.

162 Mtu *huyu* angewezaje kuhubiri Injili? Hawezi kuhubiri Injili yoyote; hakuna kitu ndani yake cha kuhubiria. Asili yake ni mwenye dhambi. Lakini Mungu alishuka akakaa ndani yake, akamfanya mwana wa Mungu, naye akaihubiri Injili. Kwa nini anaamini Neno? Kwa sababu Mungu yeye yule, aliyelifanya Neno, anahubiri moja kwa moja kupitia kwake.

163 Jinsi ninavyoliona! Je, mnaliona? Hilo hapo. Mungu yeye yule, aliyelandika Neno, yuko ndani ya huyo mtu, akisema, “Hiyo ndiyo Kweli. Sijali mtu yeyote anasema nini. Hiyo ndiyo Kweli.” Hiyo hapo. [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja.] Mungu, ndani ya mwanadamu, anatambua Neno Lake Mwenyewe. Haleluya! Hilo latosha. Mungu, *humu* ndani!

164 “Amini mambo yote. Tumaini mambo yote. Vumilia mambo yote.” Hiyo ni kweli? “Maandiko yote yamevuviwa na Mungu.” Mungu aliliandika.

165 Mungu anapoingia *humu* ndani, Mungu hutambua Neno Lake Mwenyewe, anasema, “Hakika, Hiyo ni Kweli.” Sasa, ukianza kulighushi mahali fulani, hiyo ni kati yako na Mungu. Lakini Mungu hutambua Neno Lake Mwenyewe. Amina. Loo, jinsi hilo hutufanya tujisikie, Neno la Mungu lililovuviwa! Angalieni.

166 Nilimsikia maskini mhubiri huyo Mnazarayo huko New Albany, asubuhi ya leo, akichukua huo upande mwingine wa Hilo. Ndugu, ninamaanisha aliliweka wazi pale, pia, kuhusu, “Maandiko yote yalitolewa kwa uvuvio.” Naam. Ndivyo ilivyo.

167 Sasa, Mungu ametoa ahadi, Naye akamwambia Ibrahimu yale ambayo angefanya. Alichukua kiapo Chake. Aliapa kwa nafsi Yake; hakuna aliye mkubwa zaidi. Kwa hiyo Mungu Mwenyewe. . .

168 Yote aliyokuwa, katika ile Nguzo ya Moto, alikuwa katika Kristo Yesu. “Kwa kuwa Mungu. . .” Biblia ilisema. Biblia ilisema kwamba Mungu alijifanya mtupu. . . Mnajua mnachofanya, tunapofanya kitu chochote kitupu? Alijimwaga Mwenyewe ndani ya Kristo. Hebu wazi ni tu, Mungu alijimwaga Mwenyewe ndani ya Kristo. “Naye Kristo hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa kitu cha kushikamana nacho,” kwa maana Yeye alikuwa Mungu.

169 Hilo ndilo jambo walilomwulia, “kuvunja siku ya sabato; kujifanya Mwenyewe Mungu.”

170 Naye alikuwa “Bwana wa Sabato,” Naye alikuwa Mungu, Imanueli, Kristo! “Mungu, ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Sasa, na kila kitu ambacho Mungu alikuwa, alikimwaga ndani ya Kristo.

171 Na kila kitu Kristo alichokuwa, alikimwaga ndani ya Kanisa. Kwa hiyo hivi hamwoni jinsi. . .

172 Kristo, haidhuru wanatheolojia walisema nini, Yeye alimwamini Baba. Hiyo ni kweli?

173 Walisema, “Ana kichaa!” Walisema, “Yeye ni Beelzebuli! Yeye ni ibilisi!”

174 Akasema, “Mnaweza kupita na hilo sasa, kuzungumza kunihusu Mimi. Lakini ajapo Roho Mtakatifu, msijaribu.” Mnaona?

175 Kwa kuwa, Kristo alimwamini Baba. Haidhuru walimu walisema nini, Yeye alimwamini Baba. Hiyo ni kweli? Kwa maana, Mungu alikuwa amejimwaga Mwenyewe ndani ya Kristo, nao Uungu ulikuwa ndani ya Kristo. Whiu! Natumaini mnalipata.

176 Na, basi, kile alichokuwa Kristo, Yeye alikimwaga ndani ya mwaminio wa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, haidhuru mtu yeyote anasema nini, yeye anaamini Neno la Mungu. Mnaona, hana budi kuliadini, kwa kuwa, yote aliyokuwa Kristo. Yote aliyokuwa Mungu, yalikuwa ndani ya Kristo; na yote aliyo Kristo, yako ndani yako, mwaminio.

177 Kristo hawezi kukwambia jambo fulani, asimame karibu na kulikana. Hawezi kulighairi Neno Lake. Hawezi kusema. . . Sasa, naweza kusema, naweza kusema jambo fulani; niseme, “Vema, samahani. Sikukusudia kulisema kwa njia hiyo.” Lakini,

Yeye hawezi. Hana budi kudumu na kile asemacho. Yeye ni Mungu. Hawezi kukosea, Naye hana budi kudumu na yale asemayo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Mungu, na Yeye asiyeweza kukosea, hana budi kudumu na yale aliyosema.

¹⁷⁸ Mungu alikula kiapo, akamwahidi Ibrahimu, kisha akaapa kwa nafsi Yake, ya kwamba, “Nitakuokoa Wewe na uzao wako baada yako.” Uzao wa Ibrahimu ni nini sasa? Ni nani aliye na mshiko huu thabiti? Ni nani aliyejengwa juu ya msingi huu?

¹⁷⁹ Sio tu kila Tom, Dick, na Harry. “Si wote waniambiao, ‘Bwana, Bwana, wataingia, bali yule atendaye mapenzi ya Baba Yangu aliye Mbinguni.’”

Na *Haya* ndiyo mapenzi ya Baba. *Hili* ndilo Neno Lake.

¹⁸⁰ “Wengi watakuja Kwangu, siku hiyo, na kusema, ‘Bwana, sikutabiri, na kuhubiri kwa Jina Lako? Je, sikutoa pepo kwa Jina Lako? Je, sikufanya mambo haya yote kwa Jina Lako?’ Atasema, ‘Ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu. Hata sikuwajua ninyi.’”

¹⁸¹ Mwanadamu huchochea mhemuko, na theolojia, na Kimaandiko; na kujaribu kufundisha Maandiko na kuweka tafsiri yao wenyewe Kwayo, na kusema mambo hayo hapo. “Wakiwa na mfano wa utauwa, huku wakikana Nguvu zake.”

¹⁸² Alisema, “Katika siku za mwisho, watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiopenda kufanya suluhu, wasingizaji, wasiojizuia, wenye kuwadharau walio wema,” wakiwadhihaki, kuwaita kila kitu. “Wakiwa na mfano wa utauwa,” wahubiri, wanachama, “wakiwa na mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake.” Ndivyo ilivyo. Kasema, “Hao nao mjiepushe nao. Kwa maana hawa ndio watu waendao nyumba kwa nyumba, na kuchukua mateka wanawake wajinga, wanaochukuliwa na tamaa za namna nyingi, tamaa za kila namna.” Vema, wanapiga kelele kwa kila jambo dogo linalotokea.

¹⁸³ Lakini Mkristo aliyezaliwa mara ya pili anajua mahali anaposimama. Hakuna kitakachomsukuma. Wanatembea moja kwa moja kuelekea Kalvari. Una waigaji wengi sana barabarani, hiyo ni kweli, lakini, ndugu, hiyo inaonyesha tu ya kwamba kuna mtu aliyelipata. Tuna dola za bandia na za ghushi, lakini inaonyesha tu kuna dola halisi. Dumu moja kwa moja pamoja nayo. Endelea mbele moja kwa moja.

¹⁸⁴ Ibrahimu, “Baada ya kustahimili!” Alistahimili hilo, lile pambano kuu la mateso, na kadhalika. “Alipata ile ahadi, baada ya kuvumilia.”

¹⁸⁵ Akasema, “Kama vile Yane na Yambre walivyompinga Musa.” Vema, angalieni kile ambacho Yane na Yambre wangeweza kufanya. Wangeweza kufanya karibu mambo yale yale ambayo Musa alifanya. Lakini kulikuwa na jambo moja

tu ambalo hawangeweza kufanya. Hawangeweza kuwaponya wagonjwa. Hilo ndilo jambo pekee lililoonyesha tofauti kati yao. Musa angeweza kutupa fimbo yake chini, ikageuka kuwa nyoka; vivyo hivyo na wao. Na—naye Musa angeweza kuita viroboto juu ya nchi; na wao pia. Na Musa angeweza kuleta majipu juu ya nchi; vivyo hivyo na wao. Lakini hawangeweza kuyaondoa. Wangeweza tu kuyaagiza, lakini wasingeweza kuyaondoa. Lakini, Musa angeweza, akionyesha ya kwamba Mungu ndiye mponyaji.

¹⁸⁶ Na wokovu, wao . . . uigaji wa wokovu, kugawanya wanyama vipande viwili. Ambapo, mtu yeyote anajua ya kwamba ndama na mbuzi na kondoo, na wote hao, walikuwa ni mifano ya wokovu. Kwa maana ilikuwa ni kupitia kwa matoleo ya kumwagwa kwa damu ya kondoo na mbuzi na mafahali na ndama, na kadhalika; ondoleo la dhambi.

¹⁸⁷ Lakini, alipofikia kwenye hua, mtu yeyote hapa anajua ya kwamba hua walikuwa sadaka kwa ajili ya ugonjwa. Mwenye ukoma ilibidi kutoa njiwa kwa ajili ya ugonjwa wake. Ndege alikuwa mfano wa sadaka ya wagonjwa. Na ndipo ilipofikia kuwapasua vipande viwili, la, bwana, walibaki vivyo hivyo. Hawawezi kuigwa. Hakuna . . . Hakuna kinachoweza kuponya ila Mungu. Mnaona? Ilikuwa vivyo hivyo katika Agano la Kale. Alisema, “Mimi ndimi Bwana niponyaye magonjwa yenu yote.”

¹⁸⁸ Unaweza kutoka na kutenda kama mnafiki, useme, “Loo, nimeokoka. Utukufu kwa Mungu! Naam, bwana. Nimelipata.” Nawe unaweza kuwa unadanganya. Lakini, ndugu, inapofikia wakati wa kama wewe ni mgonjwa, na kuponywa au la, hiyo inajionyesha yenyewe ni nini. Hiyo inaonyesha kama una imani, ama huna. Je, hiyo ni kweli?

¹⁸⁹ “Loo,” unasema, “Siliamini!” Hakika, huamini. Hakuna kitu ndani yako cha kuaminia, kwanza kabisa.

Angalia, sasa, unaona. Kisha, “Usininii,” kasema, “humpasui huyu.”

¹⁹⁰ Sasa angalia kilichotukia alipoonyesha upatanisho huo. Alionyesha kwamba kutakuwa na wakati ambapo wa—wataengana, vipindi hivi vya wakati, ambapo torati na neema vingetengana, wakati fulani. Alimkata mnyama vipande viwili. Alifanya haya yote.

¹⁹¹ Ndipo wakaja kwenye hua, kwa ajili ya uponyaji. Lakini Yeye ni Yeye yule.

¹⁹² Basi angalieni, chini ya—chini ya Agano la Kale pale, wakati Yane na Yambre waliposimama pale. Musa angeweza kutupa fimbo yake chini, na kuigeza kuwa nyoka; wao wangeweza, pia. Musa angeweza kuwaagiza viroboto; wao waliwaagiza, pia. Uigaji!

“Vema, tuliingia kwenye kundi hili lingine ambalo halikutenganishwa.”

¹⁹³ Ilipofikia uponyaji wa Kiungu, Musa angeweza kuponya, ama kuondoa majipu; lakini hao hawangeweza. Yaliwaambukiza, wao wenyewe, hata hivyo. Wasingeweza kuyaondoa. Wasingeweza kufanya hivyo. Walisema, “Hiki ni kidole cha Mungu.” Nao hawangeweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, mnaona, uponyaji wa Kiungu hautenganishwi. Daima imekuwa kwamba Yeye Ndiye pekee angeweza kuponya.

¹⁹⁴ Ibilisi hana nguvu hata moja ya kuponya; kamwe hajawahi kuwa nazo, ama, hawezi kuponya. Hawezi kuponya.

¹⁹⁵ Tazama. Wanafunzi wa Yesu walitoka wakaona mtu akitoa pepo. Wakasema, “Tumemwona mmoja akitoa pepo. Naye hakutufuata, nasi tukamkataza.”

¹⁹⁶ Yesu akasema, “Msifanye hivyo. Hakuna mtu, awezaye kufanya mwujiza kwa Jina Langu, akaweza kuninenea mabaya. Asiye upande wetu yu kinyume chetu. Naye asiyekusanya pamoja nasi, hutawanya.” Hiyo ni kweli? Alijua, kama mtu huyo alikuwa kabisa anapata matokeo, kwa kutoa pepo, hapana shaka alikuwa na imani thabiti kwa Mungu la sivyo ibilisi asingeweza kuona hilo. Hiyo ni kweli. Alikuwa akipata matokeo. Wengi wao walikuja na kusema walifanya, wakati hawakufanya. Lakini mtu huyu alikuwa akipata matokeo. Kweli aliwatoa, hivyo basi Yesu akasema, “Hana budi kuwa na kitu cha kiungu kumhusu, la sivyo asingeweza kufanya hivyo.” Kweli, alipata matokeo.

¹⁹⁷ Zione, zisizoweza kutenganishwa, hizo dhabihu pale! Hao hua na njiwa, naam, bwana, wasingeweza kutenganishwa. “Usiwakate vipande vipande.” Lakini, “Wapasue *hawa* vipande viwili, lakini weka kila kipande kumwelekea mwenzake,” maana torati na neema vitafungamana, moja na nyingine. Lakini, sio uponyaji; itakuwa ni vile vile wakati wote. Mnaona? Hiyo ni kweli. “Waacheni tu jinsi walivyo.”

¹⁹⁸ Sasa angalieni. Loo, jamani! Kabla hajafanya hivyo... Ibrahimu akawachinja hao wanyama na kuwaweka huko nje, naye akafanya jinsi Mungu alivyomwambia, ndipo giza likaingia. Akawafukuza ndege humo. Giza likaingia, ndege wakaenda kituoni mwao, na kadhalika. Ninii ya kutisha sana...

¹⁹⁹ Jambo la kwanza, Mungu akamlaza Ibrahimu usingizini. “Sasa, Ibrahimu, hutahusika nalo hata kidogo. Wala wewe, au uzao wako baada yako, hutakuwa na jambo hata moja la kufanya na wokovu wako mwenyewe.” Wazieni hilo.

²⁰⁰ Mungu alimwambia—alimwambia Adamu, “Kama utagusa mti huu, utaninii... Kula kutoka *Hapa*, utaishi. Ukila kutoka kwa *huo*, utakufa.” Hilo ndilo agano. Sasa, huyo ni wewe, unalo hilo jambo mbele yako, “Ukifanya *hiki*, ukifanya *kile*, uta—utakufa. Ukiishi huko, uule Huu, utaishi.” Kwa hiyo, basi, Adamu alikula kutoka kwenye *huu*, naye akafa.

²⁰¹ Neema ikamjia, ndipo Mungu akafanya agano kwa neema. Na, alipofanya hivyo, wana wa Israeli huko chini Misri. Mungu tayari alisema, kwa Neno Lake, kile atakachofanya. Alikuwa anaenda kuwatoa. Naye Mungu anawajibika kwa Neno Lake. Lakini basi wakati Mungu, huku akiwajibika kwa Neno Lake, alishuka kule na kumtuma mwokozi, Musa, neema iliwapa hilo. Huyu hapa Musa anakuja, akiwaongoza wana wa Israeli watoke, walipotoka pamoja naye.

²⁰² Wakaingia nyikani, wakasema, “Loo, tupe jambo fulani la kufanya. Tunataka kujiundia shirika, nasi tunataka utupe kitu cha kufanya. Hebu tujifanyie kitu kama hiki. Tupe torati ya kushika.” Kutoka 19 lilikuwa ndilo kosa kubwa sana ambalo Israeli waliwahi kufanya. Wakati neema ilipokuwa imeleta wokovu wao, ndipo walitaka kitu cha kufanya, ili kuustahili. Mungu tayari alimwambia Ibrahimu, kile ambacho alikuwa anaenda kufanya. Walisema, “Acheni tuwe na torati.” Na torati haikufanya hivyo; hakuna mtu (kamwe) aliyeifuata. Hawakuifuata kamwe.

²⁰³ Yesu alikuja kutimiza torati, nayo neema ilileta Mwokozi tena. Hiyo ni kweli. Kwa maana, Mungu alikuwa ameapa, haleluya, ya kwamba alikuwa anaenda kumwokoia Ibrahimu na Uzao wake.

²⁰⁴ Naye angewezaje kufanya hivyo, na waasi, wenye mioyo migumu, wenye shingo ngumu, naam, watu ambao wasingesikiliza, wala chochote kile? Walikuwa na theolojia zao zote na kadhalika, Yeye alisema. Atafanyaje jambo hilo? *Huyu* atachukua hii; na *huyu* atachukua ile. Huku Mungu akiangalia chini na kuyaona makanisa katika siku hii, jinsi wote walivyokuwa wamekusanyika pamoja, na aina hii yote ya machafuko na kadhalika. Ilimbidi kuweka njia, kwa maana aliapa ya kwamba angefanya hivyo. Si Wayahudi pekee! Alisema, “Katika wewe makabila yote ya dunia yatabarikiwa,” Myahudi, Mmataifa, vivyo hivyo. “Nitawaita Wazao.” Haleluya! Loo, jamani! “Nitawaita.” Na katika siku hii . . .

Uzao wa Ibrahimu ni nini?

²⁰⁵ “Ibrahimu alimwamini Mungu.” Chembe hii ndogo ya Damu, sehemu Yake, ilikuwa, katika kivuli, ikifanya upatanisho kwa ajili ya Ibrahimu. “Alimwamini Mungu; akahesabiwa jambo hili kuwa haki.” Mungu alimwita Ibrahimu kwa neema kuu, si kwa sababu alikuwa Ibrahimu. Alikuwa ni mwanadamu tu.

²⁰⁶ Sasa angalieni. Na kila mmoja wa watoto wa Mungu ameitwa vivyo hivyo. Huwezi kujiokoa. Hakuna unachoweza kufanya. Kama wewe ni mwenye dhambi, huwezi kumjia Mungu isipokuwa Mungu akuite. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipoitwa na Baba Yangu. Naye Baba akimwita, wote wajao, nitampa Uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho.”

207 Mungu, kwa uteuzi mkuu, ameita Uzao wa Ibrahimu. Basi, kama aina hiyo ya Uzima uliokuwa ndani ya chembe hiyo ya Damu ulikuwa juu ya Ibrahimu, ambaye aliita yasiyowezezana kwamba “yanawezezana,” akaita yasiyowezezana, kwamba, “Yangewezezana, kwa kuwa Mungu alisema hivyo.”

208 Uzao wa Ibrahimu ni watu wa aina gani?

209 Loo, msikose, msikose hili. Tafadhali msilikose. Nalisikia likija kutoka juu ya kichwa changu. Angalieni. Angalieni.

210 Basi, kama wewe ni Uzao wa Ibrahimu, huwezi kubishana na Mungu. Uzao wa Ibrahimu ni sehemu ya Roho hii. Kwa maana, Mungu alimpa Ibrahimu ishara ya tohara, kukatwa kwa nyama, kama ushuhuda Yeye alikuwa amempokea. Katika siku hizi za mwisho, amemchukua Roho Mtakatifu na kumtahiri kila mwaminio, kwa kukata mashaka yote na kutokuamini, kuamini Neno la Mungu ni safi na takatifu, Nalo ni Kweli. Tohara; kukatilia mbali kutokuamini kwote, kila kitu, kukata kila kamba inayoshikiza. Akisema, “Mungu, nakuamini; niishi au nife, nitumbukie au nizame. Ni Neno Lako. Ninaliamini.” Basi, mnaona ninachomaanisha?

211 Ndipo Mungu akasema, “Nitaapa kwa nafsi Yangu, kwa sababu hakuna niwezaye kuapa kwake.” Yeye ndiye kitu kikubwa zaidi kilichokuwapo. Alisema, “Nitaapa kwa nafsi Yangu, kwamba nitamwoko Ibrahimu na Uzao wake.” Hiyo ni kweli.

212 Sasa Uzao wa Ibrahimu ni nani? Wale waliojazwa na Roho Mtakatifu, ni Wazao wa Ibrahimu. Tazama. Tazama. Kwa Ibrahimu alikuja Isaka; kupitia Isaka akaja Kristo. Je, tunaingiaje ndani ya Kristo basi? Tunaweza tu kuwa ndani ya Kristo. . . Biblia ilisema, “Ninyi mlio ndani ya Kristo mmekufa, na mnachukua Uzao wa Ibrahimu, na ni warithi sawasawa na ahadi.” Je, hiyo ni kweli? Whiu! “Wale waliokufa katika Kristo, ndio Uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.”

213 Kwa hiyo, kupitia chembe hiyo ya Damu! Kupitia chembe yako asili ya damu, ilivunjwa, nawe umefunikwa na chembe ya Damu ya Uzao wa Ibrahimu, ambayo ni Kristo. Katika chembe hiyo ya Damu, kunaweza tu kuwa na. . . Si uovu, na uchafu, na ufisadi. Ndani ya chembe hiyo ya Damu, unaweza tu kuupata Uzima wa Mungu, ambao ni Roho Mtakatifu.

214 Nawe huwezi kuangamia zaidi ya vile Mungu Mwenyewe asivyoweza kuangamia, kwa maana ni sehemu ya Mungu. “Nitawafufua siku ya mwisho.” “Wale ambao amewahesabia haki, tayari amewatukuza.” Na Uweponi na niani mwa Mwenyezi Mungu, kila mtu aliyezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu ametukuzwa katika Uwepo Wake sasa, akingojea wakati wa ukombozi. Whiu! Jamani, jamani! Mnaliona? Mungu, kwa njia ya neema, amewaita kwa Uzao wa Ibrahimu. Na kila

mmoja wa Uzao wa Ibrahimu, Mungu Mwenyezi aliapa kwa nafsi Yake Yeye angemfufua. Mungu alisema atalishughulikia.

²¹⁵ Wewe ni Uzao wa Ibrahimu vipi? Kwa kuwa umekufa, uhai wako umefichwa, “Kwa Roho mmoja sisi sote...” sio “kuingizwa kwa njia ya barua,” sio “kuingizwa kwa kunyunyiziwa.” “Lakini kwa maji moja?” La. “Lakini kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Chembe hii ya Damu, ambayo ni Kristo Yesu.” Hapo awali, kulikuwa na Chembe moja tu ya Damu, nasi tumebatizwa mle ndani, pamoja Naye, Naye alikuwa Mwana wa Mungu. Nasi tu wana na binti za Mungu, warithi pamoja Naye katika Ufalme, tukiamini kila anachosema Baba ni Kweli. Haleluya! Ndugu!

Imani katika Baba, imani katika Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, watatu katika
Mmoja;
Pepo watatetemeka, na wenye dhambi
wataamka;
Imani katika Yehova itatemesha chochote
kile.

²¹⁶ Hiyo ni kweli. Kweli. Hiyo hapo chembe ya Damu. Ilianzia wapi? Chembe moja ya Damu. Je, hiyo ni kweli? Ni nini kilichokuwa ndani ya chembe hiyo ya Damu? Uzima wa Mungu. Ni nini ilifanyikia chembe hiyo ya Damu? Ilichomwa mkuki, na dhambi. Mkuki wa Kirumi, uliitia dhambi, ukaichoma mkuki. Kwa nini? Kwa sababu dhambi iliwekwa juu Yake. “Na ilimpendeza Mungu.” Kuhesabiwa haki kulinunuliwa papo hapo. Mungu alisema, “Hilo latosha, milele.” Hiyo hapo. Nayoy chembe hiyo ya Damu ilichomwa mkuki.

²¹⁷ Nayoy Damu ikaruka, ikanyunyizia kutoka pande zote, ile chembe ya Damu, “shuush,” ilipovunjwa pale Kalvari. Kwa sababu gani? Kuifungua chembe hiyo ambamo hakuna mtu aliyewahi kuingia hapo kabla, kuniingiza mimi na wewe kwenye chembe hiyo ya Damu; kuleta kupitia kwa Damu, “kuoshwa kwa maji ya Neno,” kwa Damu ya Kristo. “Pasipo kumwaga Damu, hakuna ondoleo la dhambi.” Kumchukua mwenye dhambi aliyepotea, kwa neema, kumvuta kupitia chembe hii ya Damu, hapa ndani, na kumpa Roho Mtakatifu. Kumvuta *huyu* huku; kumpa Roho Mtakatifu. “Nasi ni warithi pamoja na Kristo, katika Ufalme wa Mungu.” Whiu! Mungu aliye ndani yako aamke, au ujiue ili Mungu aweze kuamka, kwako, mpaka umtambue. Alikuvuta kupitia chembe ya Damu; akakuvuta kupitia kwa mnyunyizo.

²¹⁸ Ilikuwa je kwa hiyo seli ya Damu? Je, iliagamia tu na kuisha? La, bwana. Ilinyunyizia. Ilifungua. Iliwafungulia, wana wengi sana waweze kuzaliwa. La, wana wangeweza kuzaliwa kwa chembe hii moja ya Damu, Mtu huyu mmoja.

219 Roho hii moja iliingia ndani ya chembe hii ya Damu, Nayo ikaumba kumzunguka na kumzunguka Yeye, namna hiyo. Hakuna mtu, aliyewahi kuingia, kamwe wasingeweza, hapo awali. Lakini Mungu Mwenyewe alishuka na kufanyika Mtoto mchanga, horini; akatokea, na kufanywa Mtu. Haya yote, kila kitu, kilikuwa kimezungushiwa chembe hiyo moja ya Damu. Nayo ilichomwa namna hiyo, na kupasuka pale Kalvari; dhambi ikaitawanya. Mungu alimfufua kwa ajili ya kuhesabiwa haki. Sasa karibu na huyo Roho . . .

220 Roho yuyu huyu anaishi hapa duniani, leo. Naye ana mnyunyizo pande zote, namna *hii*. Sio—sio ngumu, unaweza . . . ambapo huwezi kuingia. Imefunguliwa, ili uweze kuingia ndani. Imefunguliwa, ili aweze kuingia. Kwa nini? Ili kwamba, kwa kuvutwa kwa mwenye dhambi, kupitia chembe hii ya Damu, kwake Mwenyewe . . . “Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu.”

221 Na anapomvuta mwenye dhambi huyo kupitia chembe hiyo ya Damu, Yeye humtakasa na udhalimu wote, haleluya, na kumwingiza ndani kwa njia ya Roho Mtakatifu, ndani yake Mwenyewe. Naye mwenye dhambi ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu, aliyebatizwa mle ndani na Roho Mtakatifu. Anamvuta Hapa ndani; na sehemu ya huyo mtu, Mle ndani, ni ya kiungu. Yeye ni mwana wa Mungu. Yeye ni binti wa Mungu. Tamaa zozote za ulimwengu zimekufa, maana ziko kwenye . . . Kati yake na ulimwengu ni Damu ya Yesu Kristo.

222 Kisha yeye “hutumainia mambo yote; huamini mambo yote.” Haleluya! Yale Mungu asemayo, yeye anasema, “Hiyo ni Kweli. Kuishi ama kufa, kunaleta tofauti gani? Ni Ukweli. Ninaendelea mbele.” Whiu! Samahani. Mimi—mimi kidogo sina utaratibu katika kanisa langu mwenyewe. Amina. Loo, jamani!

Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu kingine chochote

Pungufu ya Damu ya Yesu na haki;

Wakati yote yanayoizunguka nafsi yangu yakitoweka,

Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na nanga yangu.

Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;

Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

223 Iwe ni pesa, iwe ni umaarufu, iwe ni mhubiri mkubwa, iwe ni *huyu*, ama kama ni daktari, kama ni gari, ama kama ni *hili*, *lile*, ama *linginelo*! Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao! Jamani, jamani!

224 Ni zaidi sana vipi ninavyoliona, wakati ninapoona nywele zinaingia mvi, zile zilizosalia kichwani mwangu; mwili wangu ukinyauka. Tumaini langu la pekee liko Hapo.

225 Bwana Yesu, nishike mkono na kuniongoza safarini. Jalia niendeleo mbele, Bwana Mungu, nisivutiwe na chochote cha ulimwengu, lakini, “Nikimtaazama Kristo, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yangu; Ambaye kwa ajili ya walio Wake Mwenyewe, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, aliutoa uhai Wake, apate kujitoa Mwenyewe kuwa dhahibu,” apate kunileta katika ushirika pamoja Naye, katika Baba.

226 Hum! Hiyo hapo. Wenye dhambi wangewezae kamwe kulitazama Hilo na kuondoka? Ni zaidi ya chochote ninachoweza kuwazia.

227 Sawa, haraka sasa. Hatuna budi kuharakisha, kabla hatujafunga.

Tumaini tulilo nalo... (kifungu cha 19)... kama nanga ya roho, . . .

228 Hili hapa linaendelea tena, “Nanga ya roho, tumaini ambalo tunalo kama nanga.” Kitu chochote kinapotia nanga, hakiwezi kusonga.

Nina nanga inayonidumisha mzima,
Imara na hakika wakati mawimbi makubwa ya bahari yanapotanda;
Nikiwa nimetia nanga kwenye Mwamba unaonifanya mzima,
Imewekwa salama na hakika katika upendo wa Mwokozi!

229 Nanga hii! Nilipokuwa kule nje mbali na kile kioevu, siku moja; siku moja, Mungu alimchukua maskini mwenye dhambi huyu aliyepotea, na kumvuta kupitia kwenye kioevu hicho, naam, bwana, na kumleta huku na kunitia nanga mle ndani; akanikumbatia kwa mikono Yake. Na kadhalika, haijalishi ni nini, “Nafsi yangu inakutazamia Wewe!” Unaona? “Kuwa na nanga, imara na hakika.” Tazama hapa:

Tumaini tulilo nalo kama nanga ya roho, hakika na imara, . . .

230 Si kusokotwa huku na huku kwa kila fundisho na kila upepo, tukitupwa huku na huku; kuchukua upande *huku*, na kuchukua upande *huku*, wala hujui unakosimama. Biblia ilisema, “Ningependa mwimarishwe.” Sio kusema, “Vema, mimi ni—mimi ni *hivi* leo, na kitu kingine kesho yake.”

231 Itie nanga nafsi yako katika Kristo Yesu. Uzaliwe mara ya pili, Uzima wa Mungu ukiishi ndani yako, nawe unajua, bila shaka lolote, ya kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Matumaini yako yote yamejengwa pale Kalvari. Upendo wa Mungu unamiminika kupitia moyoni mwako. Nawe unaamini kila Neno ambalo Mungu anasema ni kweli. Uko tayari kufa kwa ajili ya awamu yoyote Yake. Mnaona

ninachomaanisha? “Imara na hakika!” Sasa angalieni. Hebu niisome tena.

*Tumaini tulilo nalo kama nanga ya roho, yenye hakika
na imara, liingialo hata . . . na (mnaliitaje) mlimo ndani
ya pazia;*

²³² Hiyo, nini, ndani ya pazia gani? Ninazungumza juu ya pazia gani? Pazia la Damu. Damu!

Tumevuka pazia lililopasuliwa ambamo
utukufu haushindwi,

Mnajua wimbo huo tunaoimba hapa?

Haleluya, Haleluya;
Nimevuka pazia lililopasuliwa, ile Damu,
ambapo ilipasuliwa ubavuni Mwake.

Nimevuka pazia lililopasuliwa ambapo
utukufu haushindwi,
Haleluya, Haleluya;
Ninaishi katika Uwepo wa Mfalme.

Nimevuka pazia lililopasuliwa ambapo
utukufu haushindwi.

²³³ Kama shida zangu zikija *hivi*, ama *vile*, utukufu bado haushindwi.

Nimevuka pazia lililopasuliwa ambapo
utukufu haushindwi,
Haleluya, Haleluya;
Kwa maana ninaishi katika Uwepo wa Mfalme.

²³⁴ Amenileta katika ushirika Wake, kupitia kwa upande uliopasuliwa wa Mwanawe, Kristo Yesu, amenifanya kuwa sehemu Yake; kuamini mambo yote, kumwamini Yeye, kumtumaini, kusimama pale; utukufu haushindwi kamwe. “Mambo yote yakitenda kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao,” kwa hivyo utukufu haushindwi kamwe.

Nimevuka pazia lililopasuliwa ambapo
utukufu haushindwi,
Haleluya, Haleluya;
Ninaishi katika Uwepo wa Mfalme.

²³⁵ Matumaini yangu yamejengwa Huko, si juu ya chochote pungufu. Nilikuja kwa Damu iliyoniokoa. Nilikuja kupitia Damu iliyoniponya. Chochote ninachohitaji, nikiwa humu ndani; ninaziita hizo sifa pale zije kutoka Kalvari, nazo ni zangu. Hizo ni zangu, bure. Ikiwa Baba havezi kunipa hizo, atanjulisha sababu yake. Imani yangu ingali inamtaazama Yeye moja kwa moja, ikisema, “Bwana, ninaamini kuwa unajua kilicho bora zaidi kwangu, kwa hiyo ninajikabidhi Kwako. Nami huyu hapa.” Amina. Loo, hiyo hapo. Tumaini langu ni Kwake, ndani Yake, Mungu wa Mbinguni.

²³⁶ Sasa tazama. “Wakati mtangulizi ni. . .” Loo, loo, jamani! Angalieni tu hapa, angalieni hapa! Hata sikuona hili. Angalieni kifungu hiki cha mwisho hapa, kifungu cha 20. Whiu! Ni jambo la ajabu jinsi gani!

Alimoingia mtangulizi wetu, . . . mtangulizi, Yesu, amefanywa kuhani mkuu milele kwa mfano wa Melkisedeki.

²³⁷ “Mtangulizi,” Mtu aliyetutangulia, na kama Mmoja aliyekuja na kupachukua mahali petu, si mwingine ila Mungu Mwenyewe. Alishuka na kujifanya Mwenyewe Mwanadamu, kuwa mtangulizi, ili kuwathibitishia watu.

²³⁸ Kwa nini? Aliapa, kwa kiapo, Yeye atafanya jambo hilo. Aliapa atatuokoa. Aliapa, kwamba tungeweza kufanya hivyo. Alituapia mambo haya, kwa nafsi Yake Mwenyewe.

²³⁹ Ndipo akashuka, akafanywa mtangulizi. Alijifanya Mwenyewe mtangulizi. Aliingia hapa ulimwenguni, na kuishi ulimwenguni, dhambi ikimzunguka pande zote; pasipo kutenda dhambi, kwa sababu alimwamini Mungu. Je, hiyo ni kweli?

²⁴⁰ Kisha akashuka, pia, na akafa kama mwenye dhambi, akatundikwa msalabani. Kila kitu cha kimwili kilionyesha kwamba alikuwa amekufa. Walimchapa. Wakamtundika pale juu. Vema, alivuwa damu vya kutosha, kumwua. Na kisha wakakaribia. . . Alikuwa amekufa. Mbingu zikatangaza kuwa amekufa. Dunia ikasema amekufa. Kila kitu kikasema amekufa.

²⁴¹ Yule askari wa Kirumi akamchoma mkuki moyoni Mwake, na hapo akatoa Damu Yake, “Damu na maji,” ambazo zilikuwa zimetengana, ilionyesha huzuni. Na hiyo ikasema amekufa. Maji. . . Angalieni, kama huyo Mtu alikuwa amening’inia pale, na Damu na maji yakamwagika, ilionyesha kwamba Damu na maji zimetengana. Haleluya! Alikufa. Wala kamwe hakufa kwa upanga. Kamwe hakufa kwa kule kuchomwa. Alikufa kwa sababu ya huzuni.

²⁴² Hakuna kitu duniani kitakachotenganisha damu na maji. Uliza sayansi yoyote unayotaka, au daktari yeyote. Atakwambia. Ni kupitia tu kwa huzuni kubwa mno, wakati mwingine, ambapo watu wanateseka sana hata wanaweza. . . Unajua, katika huzuni, kama huzuni kubwa na mambo kama hayo. Wakati mwingine husababisha mshtuko wa moyo, na kuwaua, wakati damu na maji zinapotengana.

²⁴³ Na hicho ndicho kilichomwua Bwana Yesu. Alikufa chini ya mikonzo ya Yehova; hiyo ni kweli, adhabu kamili, haki, kwa maana Mungu alihitaji haki. Hiyo ni kweli.

²⁴⁴ Na huko hakuna mtu angeweza kuuchukua uhai Wake. Alisema, “Nitautoa. Hakuna mtu anayeweza kuuchukua. Nitautoa, nami nitautwaa tena.”

²⁴⁵ Naye, Mungu, akionyesha kwamba kupitia kifo kigumu zaidi, katili zaidi ambacho mwanadamu angeweza kufa, Mungu alimtuma mtangulizi, Yesu Kristo. Naye akashuka hapa kama Mwanadamu. Aliishi. Akala. Akanywa. Alilia. Alilala. Alifurahi pamoja nasi, kama mwanadamu. Naye akalala pale msalabani akafa, na akapakwa dawa asioze. Kwa upanga, aliitoa ile Damu kutoka mwilini Mwake. Naye akafungwa sanda, na kuwekwa kaburini. Naye alikuwa kaburini siku tatu mchana na usiku. Nayo nafsi Yake ikaenda kuzimu, Biblia ilisema hivyo. Naam, bwana.

²⁴⁶ Lakini basi alifufuka tena. “Mungu asingeweza, asingemwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu, wala nafsi Yake kukaa kuzimu.” Ndipo akamfufua, siku ya tatu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Akampandisha Juu, kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu.

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki.

²⁴⁷ Kila kitu; kama mtangulizi! Na kwa vile Mungu alimfufua, Yeye anawajibika kwa kila mtu aliye na sehemu ya Uzima huo ndani yao, atawafufua siku ya mwisho.

²⁴⁸ Mtangulizi! Akampeleka pamoja Naye Mbinguni, akamweka mkono Wake wa kuume. Nguvu na enzi, juu sana kuliko kila mwezi, nyota, Malaika, Malaika Wakuu.

²⁴⁹ Kitu cha juu kabisa kilichowahi kuwako, kikawa kitu cha chini kabisa kilichowahi kuwako; apate kushika hicho, katikati, na kujiletea Mwenyewe, “kuupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Wakati Mungu. . . Je, mnaweza kuliwazia hilo? Kitakatifu na kilicho juu, Kitu cha juu kabisa, kilimwumba mwanadamu punde kidogo kuliko Yeye.

²⁵⁰ Mwanadamu alianguka moja kwa moja hadi *hapa*. Damu ya kondoo na mbuzi ilimshikilia umbali huu, kama uwezekano, mpaka utimilifu wa wakati ulipowadia. Ndipo Mungu akashuka, Mwenyewe; sio Malaika, si Kerubi. Lakini, Mungu alishuka kutoka Mbinguni, akaenda kuzimu; kumpandisha mwanadamu kutoka kuzimu, mpaka Mbinguni pamoja Naye. Alikuwa, akimtafuta kondoo aliyepotea. Akampata, na kumweka begani Mwake; na kupanda ngazi, leo, pamoja naye, akielekea Utukufuni. “Kama nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu.”

²⁵¹ Alikuwa Nani? Tutapata hilo Jumapili ijayo, Bwana akipenda. “Kuhani aliyefanywa kwa mfano wa Melkisedeki.” Huyu Yesu alikuwa nani? Melkisedeki. “Ambaye hakuwa na mwanzo wa siku wala mwisho wa miaka. Hakuwa na baba, hana mama.”

Ulisema, “Mariamu alikuwa mama Yake.” Loo, ndugu!

252 “Alikuwa ndiye Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Kabla ya Mariamu kuwako; Yeye alikuwako. Amina.

Ee, nataka kumwona, nataka kuutazama uso
 Wake,
 Huko nikaimbe Milele juu ya neema Yake
 iokoayo.
 Kwenye njia za Utukufuni nikainue sauti
 yangu;
 Masumbuko yote yamepita, hatimaye niko
 nyumbani, kushangilia milele.

253 “Kwa hiyo unahangaikia nini, Ndugu Branham? Kwa nini ulihibiri kwa nguvu sana? Unapoenda kwa hii . . .”

254 Loo, siwezi kuendelea, nimeridhika. Sipaswi kwenda peke yangu. Mikono hii itakuwa ya kibinadamu mara moja tu. Midomo hii itakuwa ya kibinadamu mara moja tu. Na wewe, ndugu na dada yangu, mtakuwa wanaopatikana na mauti mara moja tu.

255 Na wakati kukiwa na Roho ndani yangu, kupitia kwa mwili uliochoka na saa za uchovu, ninakulilia, ni kwa jambo moja tu, hilo ni, kukuleta katika ushirika huu hapa. Sio kukuingiza kanisani, bali kukuleta katika Kristo, kwamba, “Humo ndani mna tumaini, lililo imara na thabiti.”

256 Limetiwa nanga kwa kiapo cha Mungu. Yeye amelithibitisha, na kumpeleka mtangulizi kule, akionyesha Yeye alikuwa ni Nani. Na kumfufua, siku ya mwisho, kwenye siku ile pale, ufufuo. Iithibitisha kwamba sisi tulio ndani Yake tutatokea katika ufufuo. Na kila mtu anayepitia kwenye pazia—pazia hili sasa, uliyehesabiwa haki machoni pa Mungu, Mungu anaangalia chini na kusema, “Nimemtukuza tayari, na kumketisha kule Mbinguni.” Je, mnaliona?

257 Siwezi kukosea. Kuna Kitu ndani yangu ambacho hakitaniruhusu kufanya hivyo. Yeye hana budi . . . Loo, hakika, ningeweza kurudi kwenye maskani ndogo hapa, na kuieneza huku kote, nami na Ndugu Neville tuje pamoja hapa. Na pengine ningeweza kuwazuia watoto wangu wasife njaa. Bila shaka. Hiyo ni kweli. Ningeweza kufanya hivyo. Labda nina marafiki wa kutosha ulimwenguni, hivi leo, kama nilitaka, kusema, niende huko nje na kufanya kampeni moja kubwa kote nchini, wangenipa dola laki moja. Hizo zingenisaidia siku zangu zote, kama ningeshi kuwa na umri wa miaka mia moja. Pengine zingeniweka, ni dola laki moja, kiasi kidogo, loo, kuzigawanya tu hapa na pale, na labda tufanye utegaji kidogo, kuwinda, kitu kama hicho, kuchuma maforsadi wakati wa kiangazi. Mambo machache ya njia hiyo, ningeweza kupita nayo. Nisingelazimika kuifanya. Hiyo ni kweli. Lakini, loo, jamani! Loo, hilo hata halinibabaishi, popote!

258 Kuna Kitu fulani *hapa* ndani, kinachomtazama maskini mpagani yule kule mwenye vigutu vya mikono, mwenye ukoma, maskini kipofu huyo barabarani, mtoto huyo mdogo mwenye njaa, huku mkono wake umenyoshwa. Wataenda bila chakula cha jioni, watakaa bila kitu kingine chochote, ikiwa utawaambia tu kwamba Mtu fulani anawapenda. Ni Bwana Yesu Kristo. Wanakufa kama mbwa. Wanazikwa kwenye mahandaki, kama wanyama, pasipo kujua lolote kuhusu Mungu. Na elfu arobaini kwa siku wanakufa. Elfu arobaini kwa siku wanakufa, bila Mungu, bila Kristo, bila tumaini.

259 Ee, Mungu, ninawezaje? Laiti ningaliweza tu kukaa, kuwa mdogo zaidi, na kukaa hivyo kila wakati, mpaka Yeye atakapokuwa tayari kunichukua. Ningeweza tu kuhubiri na kuhubiri na kuhubiri, na kulia na kusihi, na kujaribu. Mnaona, Wamarekani. . . Unaweza kuwaambia chochote, wanaliadini.

260 Wamarekani, unaingia na kuanza kuwaonyesha Kweli, mahali ilipo, “Papa *Hapa!*” Nao wanatoka hapa na kujiunga na kanisa, kusema, “Vema, mimi ni mwema tu kama wewe. Sijali.” Loo, jamani!

261 Ninapoona jambo hilo, nataka kusema, “Sawa, ndugu. Hiyo ni sawa.” Lakini siwezi kulifanya.

262 Ninajua, isipokuwa awe Hapa ndani, amepotea. Amepotea. Hawezi kuokolewa; hakuna kitu huko nje cha kumwoko. Huu hapa wokovu, *hapa*, kwa njia ya kunyunyiziwa, kupitia kwa Damu, kupitia kwenye pazia lililopasuliwa. Alituleta humu na kutufanya wana na binti za Mungu. Hiyo ndiyo njia pekee, na jambo pekee nijualo. Mungu, turehemu!

263 Siku moja yatakwisha. Nitahubiri mara yangu ya mwisho; na kuifunga hiyo Biblia ya kale kwa mara ya mwisho, hiyo ni kweli, ama mojawapo. Hiyo ni kweli. Nitaimba wimbo wangu wa mwisho. Nitahubiri mahubiri yangu ya mwisho. Nitamwomba mgonjwa wa mwisho. Nitafanya kila kitu wakati mmoja, nitamalizia, na sitakuwa mtu anayepatikana na mauti tena. Magurudumu ya maisha ya kibinadamu yanazunguka hapa katika mwili wangu; yakiifanya mikono yangu ifikie, na macho yangu kutazama, na midomo yangu kunena, na kadhalika. Kila gurudumu mle ndani, likifingirika, litasimama kimya. Hivyo tu.

264 Lakini, ndugu, hicho Kitu kidogo humu ndani, kinaenda mahali pengine basi, kitapanda juu kidogo basi. Nitakuwa na mwili unaoningoja Huko juu, ambao haukuumbwa kwa mikono, bali umeumbwa kwa namna ya Mungu.

Na kwa hivyo huko Mtoni nitasimama,
Ongoza miguu yangu, ushike mkono wangu,
Bwana wa thamani, ushike mkono wangu, na
uniongoze. (Hiyo ni kweli.)

Wakati njia inazidi kuchosha, Bwana wa
thamani, kaa karibu.

²⁶⁵ Huyo Ndiye ninayetaka asimame karibu nami. Sijali kama hakuna daktari, hakuna mtu mwingine. “Bwana, simama karibu nami; ndipo haya maisha yanapokaribia kwisha, pumzi yangu inapita upesi, mapigo yangu yanapanda mkononi mwangu, mke wangu na watoto wamesimama karibu na kitanda, wakikunja mikono yao, nao marafiki zangu, wanaangalia, wakisema, ‘Loo, Ndugu Branham!’”

Mtoni nitasimama,
Ongoza miguu yangu, ushike mkono wangu,
Bwana wa thamani, ushike mkono wangu,
uniongoze.

²⁶⁶ Nayo matumaini yangu yamejengwa moja kwa moja mle ndani, ya kwamba, Yeye aliyeahidi na kuapa, kwa Ibrahimu; kama ningekubali hili, ningezaliwa mara ya pili. Mambo ya asili ya ulimwengu yangefifia. Theolojia zote za mwanadamu zingefifia. Nami ningemwamini Mungu, ningemwamini Mungu peke yake, na juu Yake ningesimama. Ninapofika mwisho wa safari hiyo, ninataka kusimama pale pale katika Nguvu hizo za kimbinguni zilizonibadilisha kutoka mwenye dhambi nikawa Mkristo. Nitamtumainia Yeye katika siku hiyo, kwa yote kwa yote yangu.

²⁶⁷ Kama wewe bado, ndugu yangu, dada, fanya hivyo leo, utafanya hivyo, tunapoomba?

²⁶⁸ Baba wa Mbinguni, tunakushukuru, kutoka vilindi vya nafsi zetu, kwa ajili ya Neno Lako. Loo, ni faraja ya jinsi gani tuliyo nayo, ya kujua kwamba matumaini yetu hayajajengwa juu ya kitu chochote pungufu ya Damu ya Yesu pamoja na haki. Wakati yote yanayonizunguka, mahali pengine popote, kila tumaini la duniani limeshindwa na kutoweka, basi tunaye Yesu. Magamba yanaanguka, vitu vya dunia vinatawanyika, kama usiku kabla ya jua, lakini Bwana Yesu anabaki vile vile katika maisha yetu.

²⁶⁹ Kama kuna mmoja hapa asubuhi ya leo, Baba, Mpendwa, ambaye hajui hakika, bila shaka lolote, kwamba wamepita kutoka mautini kuingia Uzimani! Hakuna matendo mema, hakuna kanisa, hakuna kitu kingine chochote, kiwezacho kuokoa, ni Wewe tu na Wewe peke yako. Kwamba mtu huyu. . . Baba, naomba. Na katika maneno yangu yaliyovunjikavunjika, asubuhi ya leo, singeweza kuyawasilisha jinsi ulivyoinipa Wewe. Lakini, katika njia yangu isiyo na ufasaha, ninaomba ya kwamba wanaume na wanawake katika jengo hili asubuhi ya leo wamelipokea. Mpaka, wao, wapate kujua ya kwamba hawana budi kuchujwa katika kioevu hiki cha Damu na kuletwa katika ushirika wa Mungu, warithi pamoja na Yesu, katika Ufalme wa Mungu, kwa Roho mmoja. Hakuna mwanaume aliyetusukuma. Lakini Roho ndani ya ile chembe ya Damu alituvuta, akatuvuta Kwake. Nasi twaja kupitia kwa Damu, na sasa kuingia ndani ya Kristo, katika ushirika.

270 Kama hawako Mle ndani, Baba, ingawa wao ni washiriki wa kanisa kwa miaka mingi, ingawa wamejaribu sana; Baba, wapitisha, saa ii hii, kuwaleta moja kwa moja ndani Yako, katika ushirika Wako. Kwamba, wakati uhai utakapokwisha hapa duniani, Uzima wa Milele unakaa ndani yetu, Bwana Yesu Kristo. Na jalia tufufuliwe, kama Yeye alivyofufuliwa, katika siku za mwisho.

271 Itakuwa ni masikikitiko ya jinsi gani, kuona washiriki wa kanisa na watu wamesimama pale, ambao, katika maisha yao yote, wamehangaika huku na huku, na kamwe hawajajua kuzaliwa mara ya pili ni nini hasa. Wakati, Wewe ulisema, “Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hataingia kamwe katika Ufalme.” Hangeweza kamwe, Baba, kwa kuwa hapo ndipo mahali pekee palipo na Uzima wa Milele.

272 Mitume walisema, “Twende wapi?” ulipowauliza kama walitaka kuondoka. Walisema, “Wewe peke yako unao Uzima wa milele.”

273 Ninaomba, Mungu, kwamba kila mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana, katika jengo hili asubuhi ya leo, aweze kuletwa katika ushirika huo. Kwa maana ninayakabidhi mambo haya yote Kwako, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. Amina.

274 Hiyo ni kweli, Dada Gertie.

Vipi basi? Vipi basi?

Wakati kile Kitabu kikuu kitakapofunguliwa, vipi basi? (Wazia jambo hilo.)

Wakati wale wanaoukataa Ujumbe huu leo, Wataulizwa kutoa sababu—Lini Basi?

Vipi basi? Vipi basi?

Wakati kile Kitabu kikubwa kitakapofunguliwa, vipi basi?

Wakati wale walioukataa Ujumbe huu leo, Wataulizwa kutoa sababu—Vipi Basi?

275 Ndugu, dada, haijalishi unakiri Ukristo kwa muda gani, kama huko ndani ya chembe hiyo ya Damu pamoja na Kristo asubuhi ya leo, usiache siku hii ipite. Ingia, leo. Ni yako. Sio lazima uje madhabahuni. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kulikubali. Liamini. Naye Mungu, kwa malipo, kama imani yako ni ya moja kwa moja kama Ibrahimu alivyokuwa, basi Mungu atakupua Roho Mtakatifu, kukutia muhuri katika Ufalme Wake, nawe umetiwa muhuri mpaka Siku ya Ukombozi wako. Maandiko yalisema, “Msimhuzunisha Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa huyo mmetiwa muhuri mpaka Siku ya Ukombozi wenu.”

276 Ni wangapi wanasema, “Ndugu Branham, kwa ajili yangu, ninaomba na kumtumaini Mungu ya kwamba nitakuwa mle ndani”? Hebu tuone mikono yenu. Loo, kila mahali katika jengo. “Ninamwamini Mungu kuwa hapo ndani.” Mungu akubariki.

Asilimia mia moja, Bwana. Loo, si itakuwa ya ajabu? Loo, jamani! Hebu fikiria, wakati vita vya mwisho vimepiganwa, wakati silaha zote zimepangwa, moshi wa vita umekufa, jua linatua, vitabu vimefungwa, na tunasimama kwenye Hukumu.

Vipi basi? Vipi basi?

Wakati kile Kitabu kikubwa
kitakapofunguliwa, vipi basi?

Wakati wale wanaokataa Ujumbe huu leo,
Wataulizwa kutoa sababu—Vipi Basi?

²⁷⁷ Hivi hamna furaha tumelipokea? Loo, nina furaha sana! Nina furaha sana kujua kwamba Umilele usio na mwisho nitautumia pamoja na kila mmoja wenu. Hii itakuwa tu . . .

²⁷⁸ Loo, maskini kivuli kidogo cha maskini sehemu hii ya michongoma tunayopitia ni nini? Hicho kilima kidogo kinamaanisha nini huko ng'ambo? Ni bure. Hebu tukishinde. Tusiwe kama ng'ombe bubu, wanaosukumwa sasa. Na tuwe mashujaa. Hima tutoke nje tukawachukue baadhi ya wanadamu wenzetu ambao hawamjui Yesu.

²⁷⁹ Toka ukaangalie vyumba vya pombe asubuhi ya leo; vimejaa. Angalia kila sehemu ya burudani; imejaa. Majumba ya michezo yatakuwa yamejaa, alasiri ya leo, kwa umati unaotafuta shangwe, raha, usiomjua Mungu, lakini huenda kanisani kila siku.

²⁸⁰ Hebu tufanye jambo kuhusu hilo. Twende tukawaambie wengine. Je, unataka kuwa mbinafsi vya kutosha kujua jambo hili na kuliweka katika hazina ndani yako? Mbona, la, ndugu. Hebu tuivunje, na twende mbele, tukifanya jambo lingine. Mambo makuu aliyokuwa nayo, angalia kile. . . Alishuka na kuvunja ya Kwake, ili kwamba sote tuweze kuja. Hivi haitupasi sisi, ikiwa Roho wa Mungu ndani yetu, haitupasi kuwa na nia iyo hiyo ndani yetu? Twende tukamfanye mtu mwingine kuokoka. Hebu tuzungumze nao. Je, hiyo ni kweli?

²⁸¹ Sasa je, kuna yeyote mgonjwa jengoni, anayetaka kuombewa kabla hatujafunga? Kama yupo, inua mkono wako. Vema, hapa, kwa ajili ya ndugu huyu papa hapa. Mtu mwingine? Vema, huyu hapa mwingine kule nyuma, mama yangu. Sawa, mtu mwingine? Vema, ndugu hapa nyuma. Sawa.

²⁸² Naomba ninyi nyote mje hapa sasa, na kukaa, kama mnaweza, papa hapa; tunapowaleta wazee, kama wakitaka, nasi tutawaomba.

²⁸³ Kumbukeni, katika hili, pia, kuna wokovu wa mwili: uponyaji wa Kiungu. Loo, jinsi Mungu anavyopenda kuwaponya watoto Wake!

²⁸⁴ Naam. Mzee, unayo mafuta. Sasa kama mkija tu papa hapa, mbele ya madhabahu. Asante, ndugu.

285 Kama ungefungua *Tabibu Mkuu* hapo, Dada Gertie, wakati wengine wetu, kwa unyenyekevu na utulivu, kwa muda kidogo tu sasa. “Tabibu huyu mkuu sasa yu karibu; Yesu mwenye huruma.”

286 Sasa kwa imani, ndugu zangu, na mama yangu, ingieni moja kwa moja kwenye seli hii ya Damu pamoja na Bwana Yesu, ambamo baraka hizo zote za ukombozi ni zenu. Ninyi, kila mmoja, ni Wakristo, nadhani. Na, basi, endapo ninyi ni Wakristo, mnayo haki, haki ya kisheria, kwa kila kitu ambacho Kristo alifia. Ni milki yenu. Mnaimiliki. Ni yenu.

287 Sasa, jambo pekee mnaloweza, ni kufanya kama Ibrahimu. “Baada ya kuvumilia mapigano, alipata ile ahadi.” Shetani hakuruhusu tu uichukue kirahisi. Huna budi kuwa na imani. Huna budi kuliadini. Huna budi kuvumilia.

288 Mungu aliwaambia hao. Musa alisema, “Hiyo nchi ni yenu,” na hata hivyo yote ilikuwa imezingirwa na Wafilisti na kadhalika. Akasema, “Ni yenu. Nimewapa. Sasa nendeni mkaichukue.”

289 Uponyaji wa Kiungu ni kwa kila mmoja wenu. Ni mali yenu. Sasa mnaweza kwenda kuuchukua? Nendeni, mkauchukue asubuhi ya leo. Endeni; ni yenu. Hakuna kinachoweza kuwadhuru; mko ndani ya Kristo.

290 Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, kama watumishi Wako, mzee Wako hapa anayesimama karibu nami, Bwana, tunaenda kuwapaka wagonjwa mafuta, kulingana na Neno Lako. Wewe umesema, “Waite wazee; na wawapake mafuta. Wawaombe. Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa huyo.” Na tena imeandikwa, Yesu Kristo, Maneno ya mwisho yaliyotoka katika midomo Yake mitakatifu, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ili kuthibitisha yale waliyofundisha mitume, na yale Yesu Kristo aliyofundisha, zote mbili sawa, tunaenda kuwapaka mafuta wagonjwa na kuwawekea mikono, tukiamini ya kwamba Wewe utawaponya.


291 Hawa hapa wanaume watatu wamesimama, na mama yangu mwenyewe. Nami naomba, Mungu, kwamba Roho Wako Mtakatifu ataingia moyoni mwao sasa hivi, kwa kuwa wamevutwa kupitia chembe hii ya Damu, wakaingizwa katika ushirika wa Bwana Yesu. Tukijua ya kwamba maisha haya ya kibinadamu yatasambaratika siku moja, lakini Uzima huo wa Milele utaishi milele, kuna mwili mwingine unaowangojea mara baada ya huu kwisha.

292 Lakini, Mungu, wanataka kushuhudia. Wao ni wanadamu. Hawatakuwa wa kupatikana na mauti tena, baada ya maisha haya kwisha. Na ni mara hii moja tu, na hilo latosha milele. Watakuwa wasiopatikana na mauti, tangu hapo na kuendelea. Lakini wakati wangali ni wanaopatikana na mauti na wana nafasi ya kuwaita wanadamu wenzao, Mungu, iponye miili yao,

ili waweze kutoka na kulitangaza Neno, na kuwaambia watu habari Zake. Tujalie, Bwana.

²⁹³ Juu ya misingi hii, ninaleta ombi hili Kwako, kama mtumishi Wako, au kasisi, au mhudumu. Ninawaleta Kwako, ili wapate kuishi na kuwa wazima, kwa ajili ya utukufu Wako. Nami ninawaleta kwa Damu ya Bwana Yesu. Nasi tunasonga mbele sasa kufanya yale uliyosema yafanywe. Nasi tunaisahi, kwa kufanya hivi, kila roho isiyoamini, na kuitoa kwao, ili kazi za Yesu Kristo zifanyike katika miili yao.

²⁹⁴ Baba, tunampaka ndugu yetu hapa mafuta haya, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu. (Na kumsahi adui, kwamba utoke kwake). Na jalia ugonjwa wa mwili wake uondoke, na awe na afya njema na mwenye furaha, kukutumikia Wewe. Kwa njia ya Yesu Kristo tunaomba. Amina.

²⁹⁵ Na wakati ndugu yetu anapoweka mafuta haya ya upako juu ya hiki, kichwa cha mama yangu. Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, mwanzilishi wa Uzima wa milele, na mpaji wa kila kipawa chema; uliyemfufua Mwanao, Kristo Yesu, aliyezaliwa na mwanamke, aliyefanywa, mfano wa mwili wenye dhambi; na kubeba apate kuondoa ule mwiba kutoka kwenye mauti, na kujitwika mwilini Mwake Mwenyewe maradhi ya miili yetu. Tunakubali hilo, kama tunavyofanya asubuhi ya leo. Na ni kwa ajili ya mama yangu. Na kuamini kwamba sasa, ya kwamba utamponya, tunapolitii Neno Lako. Na kama wana Wako, tunaomba kwamba roho ya ugonjwa imwache mama yangu, na awe huru kupitia kwa Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Amina. 

54-1212 Aliapa Kwa Nafsi Yake
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org